# INJILI YA UFALME WA MUNGU

*Je, unatambua kwamba Yesu alisema mwisho hauwezi kufika hadi Ufalme wa Mungu uhubiriwe ulimwenguni kote kama ushuhuda*



*"Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo – Hawatadhuru wala hawatataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu;maana dunia itajawa na kumjua BWANA,kama vile maji yanavyoifunika bahari."*
***(Isaya 11:6,9)***

BOB THIEL, PH.D.

# Injili ya Ufalme wa Mungu

## *Ndiyo Suluhisho!*

**Na Bob Thiel, Ph). D.**

Copyright©2022 by Nazarene Books.Edition 1.01. Booklet produced for the Continuing Church of God and Successors, a corporation sole. 1036 W.Grand Avenue, Grover Beach, Carlifornia, 93433, U. S. A. ISBN:978-1-63660-060-4.

**Kwa nini binadamu hawezi kusuluhisha shida zake?**

**Je! Wajua kwamba mambo ya kwanza na ya mwisho katika Biblia yaonyesha kwamba Yesu alihubiri kuhusu injili ya ufalme wa Mungu?**

**Je ! Wajua kwamba Ufalme wa Mungu ndio ulikuwa msisitizo wa mitume na wale waliowafuata baadaye?**

**Je! Ufalme wa Mungu ni nafsi ya Yesu?Je, ufalme wa Mungu ni Yesu anayeishi ndani yetu sasa hivi? Je! Ufalme wa Mungu ni aina ya ufalme halisi ujao? Je! Utaamini mambo yanayofundishwa na Biblia?**

**Ufalme ni nini? Ufalme wa Mungu ni nini? Biblia inafundisha nini? Wakristo wa Kanisa la awali walifundisha nini?**

**Je, unatambua kwamba mwisho hauwezi kuja kabla Ufalme wa Mungu hujahubiriwa kwa ulimwengu kama ushuhuda?**

*Picha kwenye jalada la mbele inaonyesha kondoo akilala pamoja na mwana-kondoo kama vile ilivyoundwa na uchapishaji na mchoro wa Burdine. Picha ilioko kwenye jalada la nyuma ni sehemu ya jengo la Kanisa la Mungu la awali lililoko Yerusalemu lililochukuliwa mwaka 2013 na Dkt. Bob Thiel.*

# YALIYOMO


1. Je, wanadamu wana suluhisho? P. 3
2. Ni injili gani Yesu alihubiri? P. 8
3. Je!Ufalme wa Mungu, ulijulikana katika Agano la Kale? P. 20
4. Je!Mitume walifundisha injili ya Ufalme? P.26
5. Vyanzo vya nje vya Agano Jipya vilifundisha Ufalme wa Mungu. P .36
6. Makanisa ya Wagiriki-Rumi yalifundisha umuhimu wa Ufalme, lakini... P.57
7. Kwa nini Ufalme wa Mungu? P.65

*Maelezo ya mawasiliano.*

# 1. Je, Wanadamu Wana Suluhisho?

Ulimwengu unakabiliana na shida nyingi.

Watu wengi wana njaa. Watu wengi wamekandamizwa. Watu wengi wanakabiliwa na umaskini. Mataifa mengi yana madeni makubwa. Watoto pamoja na wale ambao hawajazaliwa, wananyanyaswa. Magonjwa yanayoshinda dawa yanatatiza madaktari wengi. Miji mikubwa ina hewa iliyochafuliwa zaidi na haina afya. Wanasiasa wengi wanatishia vita. Mashambulizi ya kigaidi yanaendelea kutukia.

Je! Viongozi wa ulimwengu wanaweza kutatua shida zinazokabili wanadamu?

Wengi wanadhani hivyo.

## Ajenda Mpya ya Ulimwengu

Mnamo Septemba 25, 2015, baada ya hotuba muhimu ya Papa Francis wa Vatikani, mataifa 193 ya Umoja wa Mataifa (UM) walipiga kura kuyatekeleza ''Malengo 17 ya Kudumu ya Maendeleo'' ya awali yaliyopewa jina *Ajenda Mpya ya Ulimwengu. H*aya ndiyo malengo 17 ya UM:

> Lengo la 1. Kumaliza umaskini wa aina yo yote kila mahali.
>
> Lengo la 2. Kumaliza njaa, kufikia usalama wa chakula na kuimarisha lishe bora na kukuza kilimo cha kudumu.
>
> Lengo la 3. Kuhakikisha maisha bora na kuimarisha ustawi wa wote kwa umma wote.
>
> Lengo la 4. Kuhakikisha ujumla na shirika bora ya usawa na kuendeleza fursa ya elimu ya kudumu na nafasi kwa wote.
>
> Lengo la 5. Kufanikisha usawa wa jinsia na kuwezesha wanawake na wasichana wote.

Lengo la 6. Kuhakikisha uwepo na usimamizi wa kudumu wa maji na usafi wa mazingira kwa wote.

Lengo la 7. Kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya kisasa kwa bei nafuu, ya kuaminika, na kudumu kwa wote.

Lengo la 8. Kukuza, kujumuisha na kudumisha ukuaji wa uchumi, ajira ya mafanikio na heshima kwa wote.

Lengo la 9. Kujenga miundombinu thabiti, kukuza ujenzi wa viwanda unaojumuisha na kudumu na kuendeleza uvumbuzi.

Lengo la 10. Kupunguza ukosefu wa usawa ndani ya na miongoni mwa nchi.

Lengo la 11. Kufanya miji na makazi ya wanadamu ya kujumuisha, imara na ya kudumu.

Lengo la 12. Kuhakikisha matumizi na mfumo wa uzalishaji wa kudumu.

Lengo la 13. Kuchukua hatua ya dharura kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa na madhara yake.

Lengo la 14. Kuhifadhi na kudumisha matumizi ya bahari, maziwa na rasilimali ya bahari kwa maendeleo ya kudumu.

Lengo la 15. Kulinda, kurejesha na kuimarisha matumizi ya kudumu ya mazingira ya nchi kavu, usimamizi ya kudumu wa misitu, kupambana na majangwa na kusimamisha na kubadili uharibifu wa ardhi na kusimamisha kupotea kwa viumbehai.

Lengo la 16. Kukuza amani na jamii za kujumuisha kwa kudumisha maendeleo, kutoa fursa ya haki kwa wote na kujenga ufanisi, uwajibikaji na taasisi shirikishi katika ngazi zote.

Lengo 17. Kuboresha njia za utekelezaji na kuumarisha ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo ya kudumu.

Ajenda hii inadhaniwa kutekeleza kikamilifu ufikiapo mwaka 2030 na pia huitwa *Ajenda ya Maendeleo ya Kudumu ya 2030. I*nalenga kusuluhisha maradhi yanayokabiliana na wanadamu kupitia kwenye kanuni, elimu na ushirikiano wa kimataifa na madhehebu. Wakati shabaha zake ni nzuri, mbinu zake nyingine na malengo yake ni mabaya (Mwanzo 3:4). Ajenda hii, pia ni sambamba na waraka wa Papa Francis ya *Laudato Si*.

''Ajenda Mpya ya Ulimwengu'' pia inaweza kuitwa ''Ajenda Mpya ya Katoliki'' kwa vile neno ''Katoliki'' linamaanisha ''ulimwenguni kote.'' Papa Francis aliuta upitishaji wa Ajenda Mpya ya Ulimwengu ''Ishara muhimu ya matumaini.''

Papa Francis pia alisifu makubaliano ya kimataifa yanayoitwa COP21 (kinachoitwa kirasmi Mkutano wa Vyama kwa Mfumo wa Mkataba wa Mabadiliko ya hali ya hewa) mnamo Desemba 2015 na kuyashauri mataifa '' kuyafuata kwa makini njia iliyo mbele na akili inayokuwa kila wakati wa mshikamano''

Wakati hakuna anayetaka hewa iliyochafuka, kushinda njaa, kuwa maskini, kuwa katika hatari, n. K, je mshikamano huu utasuluhisha shida zinazokabili binadamu?

## Kufuatilia Rekodi ya Muungano wa Mataifa

Muungano wa Mataifa ulianzishwa na kuimarishwa mnamo tarehe 24 Oktoba, 1945, baada ya vita vya ulimwengu wa II, ili uzuie mgogoro wa aina hiyo na kujaribu kukuza amani ulimwenguni. Wakati wa uanzilishi wake, muungano huu ulikuwa na mataifa 51, yako mataifa 193 sasa hivi.

Kumekuwako na migogoro zaidi ya mia, kama sivyo, maelfu ulimwenguni tangia Muungano wa Mataifa uundwe, lakini bado hatujakuwa na tunachokiita vita vya tatu vya ulimwengu.

Wengine wanaamini kwamba ushirikiano wa kimataifa kama Muungano wa kimataifa unaodaiwa kukuzwa, ukiunganishwa na aina

ya madhehebu na ajenda ya ekumeni ambayo Papa Francis na viongozi wengi wa dini wanajaribu kuimarisha, utaleta amani na usitawi.

Hata hivyo, kufutilia rekodi ya Muungano wa Mataifa, kufanya hivi hakujakuwa vyema. Pamoja na migogoro mingi ya silaha tangia Muungano wa Mataifa uundwe, mamilioni wameishi njaa, wamekuwa wakimbizi, na/ama wamekuwa maskini hohe hahe.

Kwa muda wa mwongo uliopita, muungano wa Mataifa ulipanga kuyatekeleza *Malengo ya Maendeleo ya Milenia*. Ulikuwa na ‘’malengo manane ya maendeleo’’ lakini haya hayakufua dafu, hata kulingana na Muungano wa Mataifa (MM) mwenyewe. Kwa hivyo, mnamo 2015, ulichoitwa ‘’Malengo 17 ya kudumu ya maendeleo’’ yalipitishwa. Wengine wana matumaini. Wengine wanayachukua kama ndoto ya kubuni. Kulingana na vile ndoto ya jamii timilifu inavyoenda, mnamo Mei 6, 2016, papa Francis alisema aliota kuhusu jamii mema na timilifu ya Ulaya ambayo kanisa lake litasaidia kuifikisha. Na bado ndoto la Papa itabadilika kuwa ujinamizi. (Ufunuo 18)

**Kutakuwako na Ushirikiano fulani na Mafanikio, lakini...**

*Kamusi ya Merriam Webster* inasema kwamba jamii timilifu ni ‘’mahali panapodhaniwa kuwa kuna serikali, sheria na hali za kijamii timilifu’’

Biblia inafundisha kwamba wanadamu hawawezi kusuluhisha shida zao wenyewe:

> 23 Ee BWANA, najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu. (Yeremia 10:23)

Biblia inafundisha kwamba ushirikiano wa kimataifa hautafaulu:

> 16 Uharibifu na mashaka yamo njiani mwao. 17 Wala njia ya amani hawakuijua. 18 Kumcha Mungu hakupo machoni pao (Warumi 3:16-18).

Ijapokuwa, wanadamu wengi wanajitahidi kuelekeza mtazamo wao wa jamii timilifu na hata wakati mwingine wanahusisha dini. Lakini hakuna anayetaka kufuata njia za Mungu mmoja wa kweli.

Siyo kwamba hakutakuwako na mafanikio yo yote kwenye Muungano wa Mataifa ama malengo ya Vatikani. Kutakuwa na mengine na pia kutakuwako na vikwazo vingine.

Kwa hakika, na pengine baada ya migogoro mikubwa, aina ya mkataba wa amani utakubaliwa na kuthibitishwa (Danieli 9:27). Baadaye wengi wataamini kimakosa kwamba wanadamu wataweza kuleta jamii ya amani na timilifu.

Wengi wataamini ''mafanikio ya jamii timilifu'' hiyo (Ezekieli 13:10) pamoja na ishara tofauti na miujiza (2 Wathesalonike 2:9-12). Lakini Biblia inasema kwamba amani kama hiyo haitadumu (Danieli 9:27; 11:31-44), licha na kinachodaiwa na viongozi (Wathesalonike 5:3; Isaya 59:8).

Ikiwa wanadamu hawawezi kabisa kuleta jamii timilifu, je aina tofauti ya jamii timilifu itawezekana?

Ndiyo.

## 2. Ni Injili Gani Yesu Alihubiri?

Biblia inafundisha kwamba Jamii Timilifu inayoitwa Ufalme wa Mungu itachukua nafasi ya serikali za wanadamu (Danieli 2:44; Ufunuo 11:15; 19:1-12).

Wakati Yesu alianza huduma yake ya hadahara, alianza na kuhubiri kuhusu **injili ya Ufalme wa Mungu.** Yafuatayo ni repoti ya Marko:

> 14 Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, wakati umetimia, na Ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini Injili (Marko 1:14-15).

Neno injili, linatoka kwa neno la Kiyunani ambalo limefasiriwa kama *euangelion*, na linamaanisha ''ujumbe mzuri'' ama ''habari njema.'' Katika Agano Jipya, neno la Kiingereza la ''Ufalme'' ambalo linahusiana na ufalme wa Mungu, limetajwa karibia mara 149 katika Biblia ya kiingereza ya NKJV na mara 151 katika Biblia ya Kiingereza ya *Douay Rheims*. Linatoka kwa neno la Kiyunani linalofasiriwa kama *basileia* ambalo linaonyesha utawala ama milki ya wafalme.

Falme za wanadamu, kama vile Ufalme wa Mungu, una mfalme (Ufunuo 17:14), zinachukua eneo la kijiografia (Ufunuo 11:15), zina sheria (Isaya 2:3-4;30:9), na zina watu wanaotawaliwa (Luka 13:29).

Hapa ndipo mafundisho ya hadharani kutoka kwa Yesu ambayo Mathayo anarekodi:

> 23 Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme (Mathayo 4:23).

Mathayo pia anarekodi:

> 35 Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme (Mathayo 9:35).

Agano Jipya linaonyesha kwamba Yesu atatawala milele:

> [33] Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho (Luka 1:33).

**Luka anarekodi kwamba kusudi lililomfanya Yesu kutumwa ni kuhubiri Ufalme wa Mungu**. Kumbuka jinsi Yesu alivyofundisha:

> [43] Akawaambia, imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa (Luka 4:43).

Je, umewahi kuisikia injili hii ikihubiriwa? Je, ushagundua kwamba kusudi kuu la Yesu kutumwa ni kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu?

Luka pia anarekodi kwamba Yesu alienda na kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu:

> [10] Basi wale mitume waliporudi walimweleza mambo yote waliyoyatenda; akawachukua, akaenda nao faraghani mpaka mji mmoja uitwao Bethsaida. [11] Na makutano walipojua walimfuata; akawakaribisha, akawa akisema nao habari za ufalme wa Mungu (Luka 9:10-11).

Yesu alifundisha kwamba Ufalme wa Mungu unapaswa kuwa kipaumbele kwa wale ambao watamfuata:

> [33] Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake (Mathayo 6:33).

> [31] Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. [32] Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. (Luka 12:31-32).

Wakristo wanafaa KUUTAFUTA KWANZA Ufalme wa Mungu. Wanafanya hivi kwa kuiweka kama kipaumbele cha juu na kuishi kama Kristo angewahitaji waishi na kuangalia kurudi kwake na Ufalme wake. Na bado, wengi wanaokiri kuwa Wakristo, siyo kwamba hawatafuti kwanza ufalme pekee lakini hawajui hata ufalme huo. Wengi pia

wanaamini kimakosa kwamba kwa kushiriki katika siasa ya ulimwengu ndiyo Mungu anatarajia kutoka kwa Wakristo. Kwa kukosa kuelewa Ufalme wa Mungu, hawaishi sasa vile wanavyotakikana kuishi au hawaelewi kwa nini binadamu wamekuwa na dosari.

Kumbuka kwamba ufalme utapewa kundi dogo (Warumi 11:5). Inahitaji uvumilivu ili uwe sehemu ya kundi dogo la ukweli.

## Ufalme wa Mungu Bado Haujaanzishwa hapa Duniani

Yesu alifundisha kwamba wafuasi wake wanapaswa kuomba ili ufalme uje, lakini bado hawajaumiliki:

> 9 Baba yetu uliye mbinguni. Jina lako litukuzwe. Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe (Mathayo 6:9-10).

Yesu aliwatuma wanafunzi wake wahubiri Ufalme wa Mungu:

> 1 Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi.2 Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa (Luka 9:1-2).

Yesu alifundisha kwamba uwepo wake peke sio ufalme, kwa vile ufalme haukuwa umesimamishwa hapa duniani wakati huo:

> 28 Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. (Mathayo 12:28)

Ufalme wa ukweli utakuja wakati ujao. Haupo hapa wakati huu kama vile maandiko haya kutoka kwa Marko yanayoonyesha:

> 47 Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum (Marko 9:47).

> 23 Yesu akatazama kotekote, akawaambia wanafunzi wake, jinsi itakavyokuwa shida wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu. 24 Wanafunzi wakashangaa kwa maneno yake. Yesu akajibu tena, akawaambia, watoto jinsi ilivyo shida wenye

kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu! 25 Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. (Marko 10:23-25)

[25] Amin, nawaambia ninyi, sitakunywa tena kabisa uzao wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya katika ufalme wa Mungu (Marko 14:25).

[43] akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenyewe anautazamia ufalme wa Mungu, akafanya ujasiri... (Marko 15:43).

Yesu alifundisha kwamba ufalme kwa sasa sio sehemu ya ulimwengu huu uliopo:

[36] Yesu akajibu, ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini Ufalme wangu sio wa hapa (Yohana 18:36).

Yesu alifundisha kwamba ufalme utakuja baada ya kurudi kwake tena na kwamba yeye ndiye atakuwa Mfalme wa huo ufalme:

[31] Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu; [32] na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi [33] ataweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. [34] Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njoni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu (Mathayo 25:31-34).

Kwa vile ufalme wa Mungu haupo hapa, hatutaona ukamilifu hadi usimamishwe. Kwa sababu wengi hawaelewi Ufalme wa Mungu, wanakosa kuelewa vile serikali yake ya upendo inafanya kazi.

## Yesu Alisema ufalme umefananishwa na nini?

Yesu alitoa maelezo mengine ya kufananisha Ufalme wa Mungu:

> [26] Akasema, ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; [27] akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. [28] Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. [29] Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika (Marko 4:26-29).

> [18] Kisha alisema, ufalme wa Mungu umefanana na nini? Nami niufananishe na nini? [19] Umefanana na punje ya haradali aliyotwaa mtu akaitupa katika shamba lake, ikamea, ikawa mti; ndege wa angani wakakaa katika matawi yake. [20] Akasema mara ya pili, niufananishe na nini Ufalme wa Mungu? [21] Umefanana na chachu aliyotwaa mwanamke akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachacha wote pia (Luka 13:18-21).

Mifano hii inaonyesha kwamba, mwanzoni, ufalme wa Mungu ni mdogo, lakini utakuwa mkubwa.

Luka pia alirekodi:

> [29] Nao watakuja watu toka mashariki na magharibi, na toka kaskazini na kusini, nao wataketi chakulani katika ufalme wa Mungu (Luka 13:29).

Kwa hivyo, ufalme wa Mungu utakuwa na watu kutoka ulimwenguni kote. Hakutakuwa wa Ukoo wa Israeli pekee. Watu watakaa katika ufalme huu.

## Luka 17 na Ufalme

Luka 17:20-21 inatatiza wengine. Lakini kabla hatujafikia haya, kumbuka kwamba watu watakula katika Ufalme wa Mungu:

> [15] ‘’Heri yule atakayekula mkate katika ufalme wa Mungu’’ (Luka 14:15).

Kwa kuwa watu (katika nyakati zijazo) watakula katika ufalme wa Mungu, siyo kitu ambacho kimetengwa katika mioyo yao sasa, licha ya utafsiri mbaya/kukosa kuelewa Luka 17:21 ambacho kinapendekeza kingine.

Tafsiri ya Mofati ya Luka 17:20-21 inafaa isaidie wengine kuelewa:

> [20] Yesu alipoulizwa na Mafarisayo Ufalme wa Mungu utakuja lini, yeye akawajibu, ‘’Ufalme wa Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, [21] wala watu hawatasema, ‘’Huu hapa,’ au ‘’Ule kule,’ kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu.’’ (Luka 17:20-21, mofati)

Kumbuka kwamba Yesu alikuwa akiongea na Mafarisayo ambao hawakuwa wameongoka, wenye nia ya mwili na wanafiki. Yesu, ‘’aliwajibu,’’-Mafarisayo ndio waliuliza Yesu swali. Walikosa kumtambua.

Je, walikuwa KANISANI? Hamna!

Yesu pia hakuwa akiongea kuhusu kanisa ambalo lingeanzishwa. Na hata hakuwa akiongea juu ya hisia ya mawazo au moyo.

Yesu alikuwa akiongea juu ya UTAWALA Wake! Mafarisayo hawakumwuliza kuhusu kanisa. Hawakujua chochote kuhusu Kanisa la Agano Jipya ambalo lingeazishwa hapo baadaye. Hawakumwuliza aina ya mawazo mazuri.

Ikiwa mtu anafikiria kuwa Ufalme wa Mungu ni KANISA-na kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa ndani ya Mafarisayo-Je, kANISA lilikuwa ndani ya Mafarisayo? Hapana!

Hitimisho kama hilo ni hafifu, sivyo? Wakati tafsiri nyingine za Waprotestani zinatafsiri sehemu ya Luka 17:21 kama, ‘’Ufalme wa Mungu umo ndani yenu’’ (NKJV/KJV), hata Biblia ya Kikatoliki inayoitwa

*Biblia ya Yerusalemu Mpya* inatafsiri kisahihi kwamba ''ufalme wa Mungu u katikati yenu.''

Yesu ndiye alikuwa katikati ya Mafarisayo. Sasa Mafarisayo wakafikiria wanatarajia kuona Ufalme wa Mungu. Lakini hawakuuelewa ufalme huo. Yesu alieleza kwamba ufalme hautakuwa wa kawaida ama wa Wayahudi pekee, kama vile walivyodhani (ama Kanisa vile wengi wanavyodhani sasa). Ufalme wa Mungu hautakuwa tu kama ufalme moja kati ya falme nyingi za wanadamu na falme zinazoonekana ambazo watu wanaweza kuonyesha ama unaoweza kuonekana, na mtu kusema, ''huu ndio Ufalme,'' ama ule ndio Ufalme, ni ule pale.''

Yesu Mwenyewe alizaliwa kuwa MFALME wa huo Ufalme, vile alivyomwambia Pilato waziwazi (Yohana 18:36-37). Ujue kwamba Biblia inatumia neno ''mfalme'' ama ''ufalme'' kwa kubadilishana (k. V Danieli 7:17-18,23). MFALME wa Ufalme ujao alikuwa akisimama karibu na Mafarisayo. Lakini hawakumtambua kama mfalme wao (Yohana 19:21). Atakaporudi, ulimwengu utamkataa (Ufunuo19:19).

Yesu aliendelea mbele katika mistari inayofuata ya Luka 17, kueleza kurudi kwake mara ya pili, wakati Ufalme wa Mungu utatawala DUNIA NZIMA (tukiendelea na tafsiri ya Mofati ili tuwe na uthabiti):

> 22 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, ''Wakati utafika ambapo mtatamani kuiona moja ya siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona.23 Watu watawaambia, ''Yule kule!''Au, 'Huyu hapa!' Msiwakimbilie.24 Kwa maana Mwana wa Adamu katika siku yake atakuwa kama umeme wa radi, umulikao katika anga kuanzia mwisho mmoja hadi mwingine.25 Lakini kwanza itampasa kuteseka katika mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki. (Luka 17:22-25, mofati)

Yesu alitaja umeme wa radi kama vile alivyotaja katika Mathayo 24:27-31, akieleza kuja kwake mara ya pili KUTAWALA ulimwengu wote. Yesu hasemi kwamba watu wake hawatamwona wakati atakaporudi. Watu hawatambua kama MFALME na watajaribu kumpiga vita (Ufunuo 19:19)! Wengi watadhani Yesu anawakilisha Mpinga Kristo.

Yesu hakusema kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa ndani mwa Mafarisayo wale-aliwaambia kwamba hawatakuwa katika huo Ufalme kwa sababu ya unafiki wao (Mathayo 23:13-14). Na hata Yesu hakusema kwamba Kanisa litakuwa Ufalme.

Ufalme ni kitu ambacho wanadamu siku moja watakuja KUINGIA ndani yake-ni kama vile ufufuo wa wenye haki! Ijapokuwa hata Ibrahimu na wazee wengine wa imani hawamo humo bado (Waebrania 11:13-40).

Wanafunzi walijua kwamba Ufalme wa Mungu haukuwamo ndani yao wakati huo, na ungejitokeza kwa njia ifuatayo kama vile inavyoonyeshwa baada ya Luka 17:21:

> 11 Walipoyasikia hayo, aliongeza kusema mfano, kwa sababu alikuwa karibu na Yerusalemu, na wao walidhani ufalme wa Mungu utaonekana mara (Luka 19:11)

## Ufalme dhahiri ulikuwa wa wakati ujao

Ni jinsi gani unaweza kusema kuwa Ufalme u karibu? Katika sehemu ya kutatua swali hilo, yesu aliorodhesha matukio (Luka 21:8-28) na akafundisha:

> [29] Akawaambia mfano; Utazameni mtini na miti mingine yote.[30] Wakati iishipo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu.[31]Nanyi kadhalika, m**wonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu** (Luka 21:29-31).

Yesu alikuwa akitaka watu wake wafuate matukio ya kiunabii ili wajue wakati ufalme utakuja. Yesu mahali pengine aliwaambia watu wake kuyatazama matukio ya kuinabii (Luka 21:36; marko 13:33-37). Licha ya maneno ya Yesu, wengi hawaangalii matukio ya ulimwengu yanayohusiana na unabii.

Katika Luka 22 na 23, yesu tena alionyesha akifundisha kwamba Ufalme wa Mungu ni kitu kitakachotimilika katika wakati ujao:

[15] ''Akawaambia, nimetamani sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu;[16] kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. [17] Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi;[18] Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja'' (Luka22:15-18).

[39] Na mmoja wa wale wahalifu waliosulubiwa naye alimkufuru na kusema, ''Ukiwa wewe ni Masihi, ujiokoe na utuokoe pia.'' [40] Na mwenzake akamkemea na kumwambia,''wewe humwogopi hata Mungu?, nawe u katika hukumo iyo hiyo.[41] Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa.[42] Na akamwambia Yeshua, ''Bwana wangu unikumbuke utakapokuja katika Ufalme wako.'' [43] Lakini Yeshua alimwambia,''Amina, nakwambia leo utakuwa pamoja nami Paradiso.'' (Luka 23:39-43, kiarama katika Kiingereza sahihi)

Ufalme wa Mungu haukuja mara baada ya Yesu kuaawa kama vile Marko na Luka wanavyotuonyesha:

[43] akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenye anautazamia ufalme wa Mungu; akafanya ujasiri... (Marko 15:43).

[51] naye ni mtu wa Arimathaya, mji mmoja wa Wayahudi, tena anautazamia ufalme wa Mungu (Luka 23:51).

Kumbuka kwamba baada ya ufufuo wa kwanza ndio mtu ataweza kuzaliwa mara ya pili katika Ufalme wa Mungu kama vile Yohana anavyorekodi:

[3] Yesu, akajibu akamwambia, amin, amin nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. [4] Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee?

> Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? [5] Yesu akajibu, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu (Yohana 3:3-5).

Kumbuka kwamba baada ya Yesu kufufuka, alifundisha tena kuhusu Ufalme wa Mungu:

> [3] wale alipowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu (Matendo 1:3).

**Mahubiri ya kwanza na ya mwisho Yesu alitoa yalihusu Ufalme wa Mungu! Yesu alikuja kama mjumbe kufundisha kuhusu Ufalme**.

Yesu pia alifanya Mtume Yohana aandike kuhusu Ufalme wa Mungu wa miaka elfu ambao utakuwa duniani. Tazama alivyoandika Yohana kutoka kwa Yesu:

> [4] Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya Neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu (Ufunuo 20:4).

Wakristo wa awali walifundisha kwamba Ufalme wa Mungu wa miaka elfu utakuwa duniani na utachukua nafasi ya serikali za ulimwengu kama vile Biblia inavyofundisha (Ufunuo 5:10,11:15).

Kwa nini wengi hawajasikia zaidi kuhusu Ufalme wa Mungu ikiwa ni muhimu?

Kwa sababu Yesu aliuita siri:

> [11] Akawaambia, ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, (Marko 4:11)

Hata leo Ufalme wa Mungu ni siri kwa wengi.

Kumbuka pia kwamba Yesu alisema kwamba mwisho (wa nyakati) utakuja (mara) BAADA ya injili ya Ufalme wa Mungu kuhubiriwa ulimwenguni kote kama USHUHUDA:

> [14] Tena habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja (Mathayo 24:14).

Kuihubiri injili ya Ufalme wa Mungu ni muhimu na kunafaa kufanikishwa **katika nyakati hizi. N**i ''habari njema'' kwa vile inatoa tumaini kamili kwa maovu yote ya wanadamu, licha ya wanayoweza kufundisha wanasiasa.

**Ukizingatia maneno ya Yesu, ni wazi kwamba Kanisa la kweli linafaa kuhubiri habari njema ya Ufalme sasa. Hii ndiyo inafaa iwe kipaumbele cha Kanisa**. Ili ifanywe vizuri, lugha mbalimbali zinapaswa kutumika.

Hii ndiyo Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) linajitahidi kufanya. Na ndiyo maana kijitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha mbalimbali.

Yesu alifundisha kwamba wengi HAWATAKUBALI njia yake:

> [13] Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. [14] Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waingiao ni wachache. (Mathayo 7:13-14)

Injili ya Ufalme wa Mungu inapeleka watu kwa uzima!

Inavutia kugundua kwamba licha ya wengi wanaokiri Ukristo wanaonekana kutovutiwa na dhana kwamba msisitizo wa Kristo

ulikuwa juu ya kuhubiri injili ya Ufalme wa Mungu, wanathiolojia wa kawaida na wanahistoria wamekuwa wakielewa kwamba hiyo ndiyo Biblia inafundisha.

Na bado, yesu mwenyewe alitarajia wanafunzi wake kufundisha Ufalme wa Mungu (Luka 9:2,60).

Kwa sababu ufalme unaokuja utakuwa juu ya sheria za Mungu, utaleta amani na ustawi-na kuzitii sheria hizo katika nyakati hizi kunaleta amani ya ukweli (Zaburi 119:165; waefeso 2:15).

Na habari hizi njema ya ufalme zilijulikana katika maandiko ya Agano Jipya.

# 3. Je Ufalme Ulijulikana Katika Agano la Kale?

Mahubiri ya kwanza na ya mwisho ya Yesu yalihusu injili ya Ufalme wa Mungu (Marko 1:14-15; matendo 1:3).

Ufalme wa Mungu ni kitu ambacho Wayahudi wa nyakati za Yesu wangepaswa kujua kwa vile ulitajwa katika maandiko yao, ambayo tunayaita Agano la Kale.

## Danieli Alifundisha Kuhusu Ufalme

Nabii Danieli aliandika:

> [40] Na ufalme wanne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa
> maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama
> chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja
> na kuseta.[41] Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na
> vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu
> chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani
> yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile
> chuma kimechanganyika na udongo wa matope.[42] Na kama
> vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo,
> kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu
> yake umevunjika.[43] Na kama vile ulivyokiona kile chuma
> kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya
> nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana,
> kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo.[44] Na katika siku
> za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme
> ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine
> hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande
> vipande na kuziharibu, nao atasimama milele na milele (Danieli
> 2:40-44).

> [18] Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, na
> kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele.

> (Danieli 7:18)
>
> [21] Nikatazama na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda;22 hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme. (Danieli 7:21-22)

Kutoka kwa Danieli, tunajifunza kwamba wakati utakuja ambapo Ufalme wa Mungu utaharibu falme za ulimwengu huu na kudumu milele na milele. Tunapata pia kwamba watakatifu watakuwa na sehemu yao katika kukaribisha Ufalme huu.

Sehemu nyingi za unabii wa Danieli ni za wakati wetu katika karne hii ya 21.

Kumbuka mafungu mengine kutoka kwa Agano Jipya:

> [12] Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama. [13] Hawa wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao. 14 Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme, na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, na wateule, na waaminifu. (Ufunuo 17:12-14)

Sasa, tunaona katika Agano la Kale na Agano Jipya dhana kwamba kutakuwako na ufalme wa dunia wa nyakati za mwisho na sehemu kumi na kwamba Mungu ataziharibu na kusimamisha Ufalme wake.

## Isaya Alifundisha Kuhusu Ufalme

Mungu aliutia Isaya msukumo kuandika hivi kuhusu sehemu ya kwanza ya Ufalme wa Mungu, utawala wa miaka elfu unaojulikana kama milenia:

> [1] "Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda.[2] Na roho ya

BWANA atakaa juu yake, Roho ya hekima na ufahamu, Roho ya shauri na uweza, Roho ya maarifa na kumcha BWANA; [3] na furaha yake itakuwa katika kumcha BWANA; wala hatahukumu kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake; [4] bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili; naye ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa pumzi ya midomo yake atawauwa wabaya.[5] Na haki itakuwa mshipi wa kujifungia.[6] Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza.[7] Ng'ombe na dubu watalisha pamoja; watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe.[8] Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira.[9] Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari. [10] Na itakuwa katika siku hiyo, shina la Yese lisimamalo kuwa ishara kwa kabila za watu, yeye ndiye ambaye mataifa watamtafuta; na mahali pake pa kupumzika patakuwa na utukufu.'' (Isaya 11:1-10)

Sababu inayonifanya kutaja hii kama sehemu ya kwanza ama awamu ya kwanza ya Ufalme wa Mungu, ni kwamba katika wakati huu utakuwa wa kimwili (kabla ya mji mtakatifu, yerusalemu mpya kushuka kutoka mbinguni, ufunuo 21) na utadumu miaka elfu. Isaya alithibitisha suala la kimwili ya awamu hii wakati aliandelea kusema hivi:

[11] Na itakuwa katika siku hiyo, bwana atapeleka mkono wake mara ya pili, ili ajipatie watu wake watakaosalia, kutoka Ashuru, na kutoka Misri, na kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu, na kutoka Shinari, na kutoka Hamathi, na kutoka visiwa vya bahari. [12] Naye atawatwekea mataifa bendera, atawakutanisha watu wa Israeli, waliotupwa, atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia. [13] Na wivu wa Efraimu utaondoka, na wale

wanaomwudhi Yuda watakatiliwa mbali; Efraimu hatamhusudu Yuda wala Yuda hatamwudhi Efraimu. 14 Nao watashuka, watalirukia bega la Wafilisti upande wa magharibi; nao pamoja watawateka wana wa mashariki; watanyosha mkono juu ya Edomu na Moabu; na wana wa Amoni watawatii. [15] Na BWANA ataungamiza kabisa ulimi ya bahari ya Misri; na kwa upepo wake uteketezao atatikisa mkono wake juu ya Mto, naye ataupiga, uwe vijito saba, na kuwavuta watu wenye viatu vikavu. [16] Itakuwako njia kuu kwa mabaki ya watu wake watakaobaki, watokao Ashuru, kama vile ilivyokuwako kwa Israeli, katika siku ile waliyotoka katika nchi ya Misri. (Isaya 11:11-16).

Isaya alitiwa msukumo kuandika:

[2] Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima ya nyumba ya BWANA utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi.[3] Na mataifa mengi watakwenda na kusema, njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA katika Yerusalemu.[4] Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe... [11] Macho ya mwanadamu yaliyoinuka yatashushwa chini, na kiburi cha mwanadamu kitainamishwa, naye BWANA, yeye peke yake, atatukuzwa siku hiyo. (Isaya 2:2-4,11)

Kwa hivyo utakuwa wakati timilifu ya amani duniani. Mwishowe, nyakati hizi zitadumu milele, yesu akitawala. Kulingana na maandiko tofauti (Zaburi 90:4;92:1; Isaya 2:11; hosea 6:2), hadithi ya Wayahudi inafundisha kwamba wakati huu utadumu miaka elfu (Babylonian Talmud:Tractate Sanhedrin Folio 97a).

Isaya pia alitiwa msukumo kuandika yafuatayo:

> [6] Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake; mshauri wa ajabu, mungu mwenye nguvu, baba wa milele, mfalme wa amani.[7] Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo. (Isaya 9:6-7)

Kumbuka kwamba Isaya alisema kuwa Yesu atakuja kusimamisha ufalme na serikali. Wakati watu wanaokiri kuwa Wakristo wanataja andiko hili mwezi wa Desemba kila mwaka, wanakosa kujua kwamba linatabiri zaidi ya ukweli kwamba Yesu angezaliwa. Biblia inaonyesha kwamba Ufalme wa Mungu una serikali na sheria juu ya watawaliwa na kwamba Kristo ndiye atakayetawala. Isaya, Danieli na wengine walitabiri juu yake.

Sheria za Mungu ni njia ya upendo (Mathayo 22:37-40; Yohana 15:10) na Ufalme wa Mungu utatawaliwa kwa kutumia sheria hizi. Kwa hivyo, ufalme wa Mungu, licha ya vile wengi katika ulimwengu wanautazama, utajengwa juu ya upendo.

## Zaburi na Mengine

Sio Danieli na Isaya peke yake ndio Mungu aliwatia msukumo kuandika kuhusu Ufalme wa Mungu.

Ezekieli alitiwa msukumo kuandika kwamba wale walio wa kabila ya Israeli (sio Wayahudi pekee) waliotawanyika wakati wa Dhiki Kuu watakusanywa pamoja katika ufalme wa miaka elfu:

> [17] Basi nena, bwana Mungu asema hivi; nitawakusanya ninyi toka kati ya kabila za watu, na kuwakutanisha toka nchi zile mlizotawanyika, nami nitawapeni nchi ya Israeli. [18] Nao watafika huko, nao wataondolea mbali vitu vyake vyote

> vichukizavyo, na machukizo yake yote. [19] Nami nitawapa moyo mmoja, nami nitatia roho mpya ndani yao; nami nitaundoa moyo wa kijiwe katika miili yao, nami nitawapa moyo wa nyama;[20] ili waende katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyatenda; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.[21] Bali wao ambao mioyo yao huenda kwa kuufuata moyo wa vitu vyao vichukizavyo, na machukizo yao, nitaileta njia yao iwajilie juu ya vichwa vyao, asema Bwana MUNGU. (Ezekieli 11:17-21)

Ukoo wa kabila ya Israeli hawatatawanyika tena, lakini watatii hukumu za Mungu na kuwacha kuvila vyakula vya machukizo (Walawi 11; kumbukumbu 14).

Kumbuka yafuatayo katika Zaburi kuhusu Ufalme wa Mungu:

> [27] Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamrejea BWANA, jamaa zote za mataifa watamsujudia.[28] Maana ufalme una BWANA, naye ndiye awatawalaye mataifa. (Zaburi 22:27-28)

> [6] Kiti chako cha enzi, mungu, ni cha milele na milele, fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. (Zaburi 45:6)

> [10] Ee BWANA, kazi zako zote zitakushukuru, na wacha Mungu wako watakuhimidi. [11] Wataunena utukufu wa ufalme wako, na kuuhadithia uweza wako. [12] Ili kuwajulisha watu matendo yake makuu, na utukufu wa fahari ya ufalme wake. [13] Ufalme wako ni ufalme wa zamani zote, na mamlaka yako ni ya vizazi vyote. (Zaburi 145:10-13)

Waandishi tofauti katika Agano la Kale pia waliandika kuhusu suala la ufalme (K. V.Ezekieli 20:33; obadia 21; mika 4:7).

Kwa hivyo wakati Yesu alianza injili ya Ufalme wa Mungu, wasikilizaji wake wa karibu walikuwa wakijua baadhi ya dhana ya kimsingi ya ufalme.

# 4. Je, mitume walifundisha Ufalme wa Mungu?

Wakati watu wengi wanajifanya kwamba injili ni habari njema kuhusu nafsi ya Yesu, ukweli ni kwamba Yesu alifundisha injili ya Ufalme wa Mungu. Huo ndio ujumbe Yesu aliuleta.

## Paulo Alifundisha Ufalme wa Mungu

Mtume Paulo aliandika kuhusu Ufalme wa Mungu na Yesu:

> [8] Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu (Matendo 19:8).

> [25] Na sasa, tazameni, mimi najua ya kuwa ninyi nyote niliowahubiria ufalme wa Mungu (Matendo 20:25).

> [23] Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa utaratibu sana na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii tangu asubuhi hata jioni...[31] akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu (Matendo 28:23,31).

Kumbuka kwamba Ufalme wa Mungu hauhusu Yesu pekee (hata hivyo yeye ndiye sehemu kubwa katika ujumbe huo), kwa hivyo Paulo pia alifundisha kuhusu Yesu tofauti na alivyofundisha kuhusu Ufalme wa Mungu.

Paulo pia aliita injili hiyo kwamba ni injili ya Mungu, lakini bado ilikuwa injili ya Ufalme wa Mungu:

> [9]... Tukawahubiri hivi injili ya Mungu... [12] ili mwende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili

mwingie katika ufalme wake na utukufu wake. ( 1 Wathesalonike 2:9,12)

Paulo pia aliita kama injili ya Kristo (Warumi 1:16).''Ujumbe wa injili'' ya Yesu, ujumbe aliofundisha.

Kumbuka kwamba haikuwa tu injili kuhusu nafsi ya Yesu Kristo ama kuhusu wokovu wa mtu binafsi. Paulo alisema injili ya Kristo ni pamoja na kumtii Yesu, kurudi kwake, na hukumu ya Mungu:

> 6... Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi;7 na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na uweza wake 8 katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu;9 watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; 10 yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu(2 Wathesalonike 1:6-10).

Agano Jipya linaonyesha kwamba Ufalme ni kitu ambacho tutakipokea, sio kwamba tunao ufalme kwa wakati huu:

> 28 Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa (Waebrania 12:28).

Tunaweza kufahamu na kungojea kwa hamu kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu sasa, lakini hatujaingia ndani yake.

Paulo hasa alithibitisha kwamba mtu hawezi kuingia katika Ufalme wa Mungu na mwili wa nyama na damu, kwa sababu watu wataingia baada ya ufufuo:

> 50 Ndugu zangu, nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kutorithi kutokuharibika.51 Angalieni, nawaambieni ninyi siri; hatutalala

> sote, lakini sote tutabadilika,[52] kwa dakika moja kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na watu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. (1 Wakorintho 15:50-52)

> 1 Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake ( 2 Timotheo 4:1).

Paulo hakufundisha hayo peke yake lakini aliongeza kwamba Yesu atampa Mungu Baba Ufalme:

> [20] Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuka lao waliolala.[21] Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu,[22] Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.[23] Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja.[24] Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu.[25] Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. (1 Wakorintho 15:20-25)

Paulo pia alifundisha kuwa wasio na haki (wavunja amri) hawataridhi Ufalme wa Mungu:

> [9] Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; washerati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wasinzi wala wafiraji, wala walawiti,[10] wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi. (1 Wakorintho 6:9-10)

> [19] Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi,[20] ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi,[21] husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayohusiana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu

watendao mambo ya jinsi hiyo, hawatauridhi ufalme wa Mungu. (Wagalatia 5:19-21).

[5] Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu. (Waefeso 5:5).

Mungu ana viwango na anataka toba kutoka kwa dhambi ili uweze kuingia katika Ufalme wake. Mtume Paulo alionya kwamba wengine hawatafundisha haya:

[6] Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine.[7] Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo.[8] Lakini ijapokuwa sisi ama malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na aalaniwe.[9] Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na aalaniwe. (Wagalatia 1:6-9)

[3] Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo.[4] Maana yeye ajaye akihubiri Yesu mwingine ambaye sisi hatukumhubiri, au mkipokea roho nyingine msiyoipokea, au injili nyingine msiyoikubali, mnatenda vema kuvumilia naye! (2 Wakorintho 11:3-4).

Ni nini ilikuwa injili ''nyingine'' au ''tofauti'' ya uwongo?

Injili ya uwongo ina sehemu nyingi tofauti.

Kwa jumla, injili ya uwongo ni kuamini kwamba hakuna haja ya kumtii Mungu na kujaribu kuishi katika njia yake ya ukweli wakati bado unajidai kumjua Mungu (Mathayo 7:21-23). Huwa ni injili ya ubinafsi.

Shetani alidanganya Hawa katika injili ya Uwongo karibia miaka elfu 6,000 iliyopita (Mwanzo 3)-na watu wameamini kwamba wanajua kumliko Mungu na wanapaswa kuamua mema na mabaya peke yao bila Mungu. Ndiyo, baada ya kuja kwa Yesu, jina lake limekuwa likiambatanishwa na injili tofauti ya uwongo-na hii imeendelea na bado itaendelea hadi wakati wa Mpinga Kristo wa mwisho.

Kwa hivyo katika nyakati za Paulo, injili ya uwongo ulichanganywa na maarifa ya siri ya ukweli na urongo. Watu wenye maarifa haya ya siri kimsingi waliamini maarifa ndiyo yalihitajika ili ufikie ufahamu hata ya wokovu. Waliamini kwamba kilichofanywa na mwili hakikuwa na madhara yo yote na walipinga kumtii Mungu katika masuala kama kutunza siku ya saba ya Sabato. Moja kati ya viongozi hao waongo ni Simoni Magusi, aliyeonywa na Mtume Petro (Matendo 8:18-21).

## Lakini sio Rahisi

Agano Jipya linaonyesha kwamba Filipo alifundisha Ufalme wa Mungu:

> 5 Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo... 12 Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu... (Matendo 8:5,12).

Lakini Yesu, paulo na wanafunzi walifundisha kwamba sio rahisi kuingia katika Ufalme wa Mungu:

> 24 Yesu alipoona vile alisema, kwa shida gani wenye mali watauingia ufalme wa Mungu! 25 Kwa maana ni vyepesi ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.26 Nao waliosikia walisema, ni nani basi awezaye kuokoka? 27 Akasema, yasiowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu. (Luka 18:24-27)

22 ''imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.'' (Matendo 14:22)

> 3 Ndugu, imetupasa kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, kama ilivyo wajibu, kwa kuwa imani yenu inazidi sana, na

> upendo wa kila mtu kwenu kwa mwenzake umekuwa mwingi.[4] Hata na sisi wenyewe twaona fahari juu yenu katika makanisa ya Mungu kwa ajili ya saburi yenu, na imani mliyo nayo katika adha zenu zote na dhiki mnazostahimili.[5] Ndiyo ishara hasa ya hukumu iliyo haki ya Mungu, ili mhesabiwe kuwa mwastahili kuuingia ufalme wa Mungu, ambao kwa ajili yake mnateswa.[6] Kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi; [7] na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake (2 Wathesalonike 1:3-7).

Kwa sababu ya ugumu, wengine wanaitwa na kuchaguliwa kwa wakati huu ili wawe sehemu ya Ufalme huo (Mathayo 22:1-14; Yohana 6:44; waebrania 6:4-6). Wengine wataitwa baadaye, kama vile Biblia inaonyesha kwamba ''Hao nao wakosao rohoni mwao watapata kufahamu, na hao wanung'unikao watajifunza elimu '' (Isaya 29:24).

## Petro Alifundisha Ufalme

Mtume Petro alifundisha kwamba ufalme ni wa milele, na kwamba injili ya Mungu lazima watu waitii kwa bidii la sivyo kutakuweko na hukumu:

> [10] Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo, hamtajikwaa kamwe.
> [11] Maana hivi mtaruzukiwa kwa karimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo. (2 Petro 1:10-11)

> [17] Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? (1 Petro 4:17)

## Vitabu vya Mwisho vya Biblia na Ufalme

Biblia hufundisha kwamba ''Mungu ni upendo'' (1 Yohana 4:8,16) na Yesu ni Mungu (Yohana 1:1,14)-Ufalme wa Mungu utakuwa na Mfalme

ambaye ni upendo ambaye sheria zake zinatekeleza upendo, sio chuki (Ufunuo 22:14-15).

Kitabu cha mwisho hasa kinazungumza kuhusu Ufalme wa Mungu.

> 15 Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele. (Ufunuo 11:15).

Yesu atatawala katika Ufalme huu! Na Biblia inafunua majina yake mawili:

> 16 Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, mFALME WA WAFALME, nA BWANA WA MABWANA (Ufunuo 19:16).

Lakini je ni Yesu peke yake atakayetawala? Kumbuka fungu hili kutoka kwa Ufunuo:

> 4 Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu... 6 Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu. (Ufunuo 20:4,6)

Wakristo wa ukweli watafufuliwa ili watawale pamoja na Kristo miaka elfu! Kwa sababu Ufalme utadumu milele (Ufunuo 11:15), lakini utawala uliotajwa ni ya miaka elfu. Hiyo ndiyo maana nilitaja hapo awali ya kwamba hii ni awamu ya kwanza ya ufalme-ya kawaida au kimwili, ya miaka elfu ikilinganishwa na awamu ya mwisho ambayo ni ya kiroho zaidi.

Matukio machache yameorodheshwa yakifanyika kati ya miaka elfu na awamu za mwisho ya Ufalme wa Mungu:

> [7] Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, shetani atafunguliwa atoke kifungoni mwake;[8] naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari... [11] Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, Cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. [12] Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima, na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. [13] Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa watu waliokuwamo ndani yake. [14] Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. [15] Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto. (Ufunuo 20:7-8,11-15)

Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha kwamba kutakuwako na awamu ya mwisho ambayo inakuja baada ya utawala wa miaka elfu na baada ya mauti ya pili:

> [1] Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.[2] Nami nakauona mji ule mtakatifu, yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.[3] Nikasikia sauti kubwakutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.[4] Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo

tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. (Ufunuo 21:1-4)

> [1]Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo,[2] katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao aina ya matunda aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi, na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.[3] Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake;[4] nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.[5] Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. (Ufunuo 22:1-5)

Kumbuka kwamba utawala huu, ambao utakuwa baada ya miaka elfu, ni pamoja na watumishi wa Mungu na unadumu milele. Mji Mtakatifu, ambao unaandaliwa mbinguni, utaacha mbingu na kushuka hapa duniani. Hii ndiyo mwanzo wa awamu ya pili ya Ufalme wa Mungu. Wakati AMBAPO HAPATAKUWA NA MAUMIVU NA MATESO!

Wapole wataurithi dunia (Mathayo 5:5) na kila kitu (Ufunuo 21:7)). Dunia, pamoja na Mji Mtakatifu ambao utakuwa juu yake, vitakuwa vyema kwa sababu njia za Mungu zitatekelezwa. Tambua kwamba:

[7] Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe (Isaya 9:7).

Kwa wazi kutakuwako na ukuaji baada ya awamu ya mwisho ya Ufalme wa Mungu kuanzishwa kwa sababu wote watatii serikali ya Mungu.

Huu utakuwa wakati wa utukufu mno:

> [9] lakini, kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia

wampendao. [10] Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. ( 1 Wakorintho 2:9-10)

Ni wakati wa upendo, furaha, na faraja wa milele. Utakuwa wakati wa ajabu!

Je, unataka kuwa katika sehemu ya Ufalme huu?

# 5. Vyanzo nje ya Agano Jipya vilifundisha Ufalme wa Mungu

Je, maprofesa wa Kristo walifikiri kwamba walipaswa kuhubiri injili ya Ufalme halisi wa Mungu?

Ndiyo.

Miaka iliyopita, katika mhadhara uliotolewa na Profesa Bart Ehrman wa Chuo Kikuu cha Carolina Kaskazini, alirudia na kwa usahihi, alisisitiza kwamba kinyume na wanaokiri kuwa Wakristo leo, yesu na wafuasi wake wa awali, walitangaza Ufalme wa Mungu. Hata kama, kuelewa kwake kwa jumla ya Ukristo kunatofautiana sana na Kanisa la Mungu Lianaloendelea (CCOG), tunaweza pia kukubali kwamba wengi wanaokiri kuwa Wakristo leo hawaelewi ufalme.

## Maandishi na Mafundisho ya Kitambo yaliyohifadhiwa baada ya Agano Jipya

Ufalme wa Mungu ulikuwa sehemu muhimu ya iliyodaiwa kuwa ‘’mahubiri yaliyo kamili ambayo yamedumu’’ (Holmes M. W. Ancient Christian Sermon. The Apostolic Fathers:Greek Texts and English Translations,2nd ed. Baker Books, Grand Rapids,2004, p. 102). Mahubiri haya ya Ukristo yalikuwa na maelezo kuyahusu:

> 5.5 Zaidi ya hayo ndugu zangu, mwajua, kwamba kuishi kwetu katika ulimwengu wa mwili hakuna maana na ni ya mapito, lakini ahadi ya Kristo ni kubwa na ya ajabu:kupumzika katika ufalme unaokuja na uzima wa milele.

Maelezo hayo ya juu yanaonyesha kwamba ufalme sio wa wakati huu, lakini utakuja na utadumu milele. Zaidi ya hapo, mahubiri haya ya zamani yanaeleza:

> 6.9 Ikiwa sasa hata wenye haki kama hawa hawawezi kupitia kwa matendo yao ya haki, kuwaokoa watoto wao, ni uhakika

gani tunao wa kuingia katika ufalme wa Mungu ikiwa tumeshindwa kutunza batizo yetu iwe safi na bila dosari? Au nani atakuwa mtetezi wetu, ikiwa hatutapatikana kuwa watakatifu na wenye kazi za haki? Kwa hivyo tupendane, ili tupate kuingia katika ufalme wa Mungu. 1[1.7]Kwa hivyo, ikiwa tunajua kilicho chema machoni pa Mungu, tutaingia katika ufalme wake na kuzipokea ahadi ambazo 'sikio halikuyaona, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu.''

> [12. 1]Wacha tuungoje kila wakati ufalme wa Mungu katika upendo na haki, kwa sababu hatujui siku atakapotokea. [12.6]anasema ufalme wa Baba utakuja.

Maelezo hayo ya juu yanaonyesha kwamba upendo kupitia kwa kuishi kwa njia ifaayo inahitajika, kwamba bado hatujaingia katika ufalme bado, na kwamba utafanyika wakati Mungu atajitokeza-yaani baada ya Yesu kurudi tena. Ni ufalme wa Baba na ufalme sio Yesu tu.

Ni ya ajabu kwamba mahubiri ya kitambo sana ambayo Mungu ameruhusu yaendelee kudumu pia yanafundisha Ufalme wa Mungu ambao Agano Jipya linafundisha na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) pia linafundisha (mafundisho haya yanawezakuwa yametoka kwa Kanisa la Mungu halisi, lakini maarifa yangu haba ya Ugiriki yamezuia uwezo wangu wa kutoa tamko iliyo imara)

## Viongozi wa Karne ya Pili na Injili ya Ufalme

Inafaa ijulikane kwamba katika karne ya 2 Papiasi, msikilizaji wa Yohana na rafiki wa Polycarpu na aliyejulikana kama mtakatifu wa Katoliki, alifundisha ufalme wa miaka elfu. Usebi alirekodi kwamba Papiasi alifundisha:

> ... Kutakuwako na miaka elfu baada ya ufufuo wa wafu wakati utawala wa Yesu utasimamishwa hapa duniani. (Fragments of Papias, vI. See also Eusebius, Church History, book 3,XXXIX,12).

Papiasi alifundisha kwamba wakati huu utakuwa wakati wa wingi:

> Kwa jinsi hiyo, (Alisema) ndiyo mbegu ya ngano itazaa masuke elfu, na kwamba kila suke litazaa mbegu elfu kumi, na kila mbegu itazaa pauni kumi ya unga ulio safi, mzuri, halisi na kwamba tufaha na mbegu na nyasi zitazaa katika kiwango kilicho sawa; na kwamba wanyama wote wanaokula kutoka kwa mazao ya ardhi, watakuwa wapole na wastaraabu, na watakuwa chini ya uongozi timilifu ya mwanadamu. [Ushuhuda umetolewa kwa mambo haya katika maandiko ya Papiasi, mtu wa zamani aliyekuwa msikilizaji wa Yohana na rafiki wa Polycarpu, katika kitabu chake cha nne; kwa vile vitabu vitano vilitungwa na yeye...] (Fragments of Papias, iV)

Barua iliyoandikiwa Wakorintho baada ya Agano Jipya inasema:

> [42:1-3]Mitume waliipokea Injili kwa ajili yetu kutoka kwa Bwana Yesu Kristo; Yesu Kristo alitumwa kutoka kwa Mungu, na mitume wametoka kwa Kristo. Wote basi walikuja kwa mapenzi ya Mungu kwa mpango ulioteuliwa. Baada ya kupata ujasiri na baada ya kuwa na uhakika kupitia kwenye ufufuo wa Bwana wetu Yesu Kristo na kuthibitishwa katika neno la Mungu na hakikisho ya kutosha ya Roho Mtakatifu, waliendelea mbele wakitangaza habari njema kwamba ufalme wa Mungu unapaswa kuja.

Polycarpu wa Smina alikuwa kiongozi wa awali wa Wakristo, ambaye alikuwa mwanafunzi wa Yohana, mtume aliyekufa wa mwisho katika mitume wa awali. Polycarpu c. 120-135 B. K. alifundisha:

> Heri walio maskini na wale wateswao kwa ajili ya haki, maana ufalme wa Mungu ni wao. (Polycarp. Letter to the Phillipians, Chapter II. From Ante-Nicene Fathers, volume 1 as edited by Aleksander Roberts & James Donaldson. American Edition,1885).

> Tukijua kwamba ''Mungu hajaribiwi,'' tunapaswa kutembea kulingana na amri zake na utukufu wake... Kwa sababu ni vyema wakiepukana na tamaa iliyo ulimwenguni kwa vile ''kila tama hupingana na roho;'' na ''wasinzi, wala wafiraji, na wanaojichafua wenyewe na wenzao, hawataurithi ufalme wa Mungu wala wale wanaofanya vitu kinyume na vinavyopotosha. (sawa na hapo, sura V).
>
> Wacha na tumtumikie kwa hofu, na heshima, hata vile yeye mwenyewe alivyoamuru, kama vile mitume waliotuhubiria Injili, na manabii waliotutabiria kitambo kuhusu kuja kwake Bwana. (sawa na hapo, sura VI)

Kama na wengine walio katika Agano Jipya, polycarpu alifundisha kwamba wenye haki, sio wavunja amri, wataurithi Ufalme wa Mungu.

Yafuatayo pia yanadaiwa kufundishwa na Polycarpu:

> Na Sabato iliyofuata alisema; 'Sikieni himizo langu, watoto wa Mungu wapendwa. Niliwapisha wakati maskofu walikuwepo, na sasa tena nawahimiza nyote mpate kutembea kistahifu na inavyostahili katika njia ya Bwana... Kesheni na pia mwe tayari, mioyo yenu isichoke, amri mpya kuhusu kupendana ninyi kwa ninyi, kwa sababu kurudi kwake kwa ghafula kutatokea kama radi, hukumu kubwa ya moto, uzima wa milele, ufalme wa kiroho. Na yote yaliyofundishwa kuhusu Mungu mnafaa mjue kupitia katika maandiko matakatifu, yakiandikwa katika mioyo yenu na Roho Mtakatifu ili amri ikae ndani yenu bila kufutika.' (Life of Polycarp, Chapter 24. J. B. Lightfoot, the Apostolic Fathers, vol.3.2,1889, pp.488-506)

Melito wa Sarde, aliyekuwa kiongozi wa Kanisa la Mungu, mnamo 170 B. K., alifundisha:

> Kwa kweli amri imetolewa katika injili-ya kale ndani ya ile mpya, zote zinazotoka pamoja Sayuni na Yerusalemu; na torati

> iliyotolewa katika neema, na aina yake iliyowekwa katika njia iliyokamilishwa na mwana kondoo katika Mwana, na kondoo katika binadamu na mwanadamu ndani ya Mungu...

Lakini injili ikawa maelezo ya sheria na utimizaji wake, wakati kanisa likawa ghala ya ukweli...

> Huyu ndiye aliyetuokoa toka utumwani hadi kwa uhuru, toka gizani hadi kwa nuru, toka kwa mauti hadi uzimani, toka kwa udhalimu hadi ufalme wa milele. (Melito. Homily On the Passover, verses 7,40,68. Translation from Kerux:The Journal of Online Theology http://www. Kerux.com/documents/KeruxV4N1A1. Asp).

Kwa, hivyo Ufalme wa Mungu ulijulikana kama kitu cha milele, na sio tu Kanisa la Katoliki ama Wakristo wa sasa na utakuwa na sheria.

Maandiko mengine ya katikati ya karne ya pili yanahimiza watu kutazamia ufalme:

> Kwa hivyo msiache mtu ye yote awatawanye tena ama msiangalie nyuma, na kwa hiari tukaribie Injili ya Ufalme wa Mungu. (Roman Clement.Recognitions, book X, Chapter XLV.Excerpted from Ante-Nicene Fathers, volume 8. Edited by Aleksander Roberts & James Donaldson. American Edition,1886)

Zaidi ya hayo, wakati haikuwahi kuandikwa kwa dhahiri na mtu ye yote katika Kanisa la kweli, maandiko ya katikati ya karne ya pili yaliyopewa mada *Mchungaji wa Hermasi* katika tafsiri na Robert na Donaldson linatumia neno ‘Ufalme wa Mungu’ mara kumi na nne.

Wakristo wa ukweli, na hata wengi wanaokiri Kristo, walijua kitu kuhusu Ufalme wa Mungu katika karne ya pili.

Hata mtakatifu Ireni wa Katoliki na Othodoksi wa Mashariki alielewa kwamba baada ya ufufuo, wakristo wataingia katika Ufalme wa Mungu. Tazama alichoandika mnamo, k. 180 B. K:

> Kwa maana hiyo ndiyo hali ya wanaoamini, kwa vile ndani yao hukaa Roho Mtakatifu, waliopokea wakati wa Batiso na imehifadhiwa na aliyeipokea, ikiwa atatembea katika ukweli na utakatifu na haki na uvumilivu wa subira. Kwa maana roho hii ina ufufuo ndani yao wanaoamini, mwili kuupokea roho tena, na pia kupitia nguvu za Roho Mtakatifu anafufuliwa na kuingia katika ufalme wa Mungu. (Irenaeus, st. Bishop of Lyon. Translated from the Armenian by Armitage Robinson. The Demostration of the Apostolic Preaching, Chapter 42. Wells, somerset, Oct. 1879. As published in SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE. NEW YORK:THE MACMILLAN CO,1920).

## Shida katika Karne ya Pili na Tatu

Licha ya kukubali kulikoenea kote katika karne ya pili, kiongozi mpinga sheria aliyeitwa Marcion alichipuka. Marcion alifundisha dhidi ya sheria za Mungu, sabato, na Ufalme wa Mungu. Hata kama alikemewa na Polycarpu na wengine, alikuwa na uhusiano na Kanisa la Rumi kwa muda na pia alikuwa na ushawishi hapo.

Katika karne ya pili na ya tatu waistiari walikuwa wamefahamika katika mji wa Aleksandria (Misri). Waistiari wengi walipinga mafundisho ya ufalme unaokuja. Tazama ripoti iliyoandikwa na baadhi ya waistiari:

> Dionisi alizaliwa na familia ya pagani waliokuwa na heshima katika mji wa Aleksandria, na kuelimishwa katika filosofia yao. Aliacha shule za wapani ili awe mwanafunzi wa Origeni, ambaye alichukua nafasi yake baadaye kuwa kiongozi wa shule ya katekesi wa mjini Aleksandria...

> Clementi Origeni na Shule ya Uignostiki walikuwa wakichakachua mafundisho ya mausia matakatifu na ufafanuzi wao wa kistiari... Walijipokea jina ''waistiari.''Neposi alipambana na waistiari waziwazi aliposisitiza kwamba kutakuwako na utawala wa Kristo hapa duniani...
>
> Dionisi alibishana na wafuasi wa Neposi na kwa maelezo yake...'' kwa hali ya vitu hivyo sasa vimekuwepo katika ufalme wa Mungu.'' Hii ndiyo mara ya kwanza ufalme wa Mungu umetajwa kwamba unapatikana sasa hivi katika makanisa...
>
> Neposi alikana upotofu wao akionyesha kwamba ufalme wa mbinguni sio istiari, lakini ni ufalme unaokuja wa Bwana wetu katika ufufuo wa uzima wa milele...
>
> Kwa hivyo dhana ya ufalme kuwepo katika hali ya vitu vya kisasa ililetwa na kuendelezwa na shule ya wagnostiki waistiari katika Misri,200 hadi 250 B. K, karne mzima kabla ya maaskofu wa utawala hawajazingatiwa kuwa wamiliki wa enzi...
>
> Clementi alielewa dhana ya ufalme wa Mungu kama hali kamili ya kuwa na akili ya kumjua Mungu.Origeni alieleza ufalme kama maana ya ndani ya kiroho iliyofichwa katika maandiko . (Ward, henry Dana. Ufalme wa Mungu:Ufalme usio wa ulimwengu huu; haupo kwa ulimwengu huu, lakini unakuja katika nchi ya mbinguni, wa ufufuo kutoka kwa wafu na ya kuwekwa kila kitu sawa. Ulichapishwa na Caxyton, Remsen & Hafflelfinger,1870. Uk. 124-125)

Kwa hivyo, wakati Askofu Neposi alikuwa akifundisha ufalme wa Mungu, waistiari walijaribu kuleta injili ya uwongo, isiyo halisi kuhusu ufalme. Askofu Apollinaris wa Hiropoli pia alijaribu kuyapiga vita makosa ya waistiari wakati huo. Wale walioko katika Kanisa la Mungu walisimama katika ukweli wa Ufalme wa Mungu halisi katika vipindi vyote vya historia.

## Herbert W. Armstrong Alifundisha Ufalme wa Mungu, pamoja na

Katika karne ya 20, hayati Herbert W. Armstrong aliandika:

> Kwa sababu walikataa Injili ya Kristo..., ulimwengu wangeleta kitu kingine kichukie nafasi yake. Wangebuni injili bandia! Kwa hivyo tumesikia ufalme wa Mungu ukisemwa kama maelezo ya kawaida tu –hisia nzuri katika mioyo ya wanadamu---wakiupunguza kama ya peponi, isiyo halisi na HAUNA MAANA! Wengine wamekosea kwamba ''KANISA'' ndio ufalme... Nabii Danieli aliyeishi miaka 600 kabla ya Kristo, alijua kwamba ufalme wa Mungu ni ufalme halisi---serikali itakaotawala watu halisi hapa duniani...
>
> Hapa... Ni maelezo ya Mungu vile UFALME WA MUNGU UTAKUWA ''Na katika siku za wafalme hao...'' hapa panaongea kuhusu vidole kumi, nusu ya chuma na nusu ya udongo. Haya ukiunganisha unabii huu na Danieli 7, na Ufunuo 13 na 17, unaashiria MUUNGANO mpya WA ULAYA ambao unaundwa sasa... Mbele ya macho yako! Ufunuo 17:12 inaeleza wazi kwa undani kwamba utakuwa muungano wa WAFALME KUMI AMA FALME na (Ufunuo 17:8) utafufua UTAWALA WA RUMI ule wa kale...
>
> Wakati Yesu atakaporudi, atarudi kama MFALME wa wafalme, akitawala dunia nzima (Ufunuo 19:11-16); na UFALME WAKE---UFALME WA MUNGU, Danieli alisema, UTAZIHARIBU falme zote za ulimwengu. Ufunuo 11:15 inaeleza ufalme kwa maneno haya: ''ufalme wa dunia umekwisha kuwa UFALME WA BWANA WETU NA WAKRISTO WAKE, naye atamiliki hata milele na milele''! Huo ndio UFALME WA MUNGU. Utakuwa MWISHO wa serikali za kisasa, ndiyo na hata mwisho wa Marekani na mataifa ya Uingereza. Baadaye zitakuwa falme ---SERIKALI---ya Bwana wetu YESU KRISTO, atakayekuwa MFALME wa wafalme duniani kote. Haya yanaweka wazi

hakika ILIYO WAZI kwamba UFALME WA MUNGU ni SERIKALI halisi. Kama vile utawala wa Wakaldayo ulikuwa UFALME---kama vile Utawala wa Rumi ulikuwa UFALME---kwa hivyo UFALME WA MUNGU ni serikali. Inapaswa kuchukua nafasi ya SERIKALI za MATAIFA ya ulimwengu. Yesu ALIZALIWA ili awe MFALME---MTAWALA!...

Na Yesu mwenyewe aliyetembea juu ya milima na nyufa za Nchi Takatifu na kwenye mitaa ya Yerusalemu zaidi ya miaka 1,900 iliyopita anakuja tena. Alisema atakuja tena. Baada ya kusulubishwa, mungu alimfufua kutoka kwa wafu baada ya mchana tatu na usiku tatu (Mathayo 12:40; matendo 2:32;I Wakorintho 15:3-4). Alipaa na kuketi katika kiti cha enzi cha Mungu. Makao makuu ya Serikali ya Mungu kule mbinguni (Matendo 1:9-11; waebrania 1:3;8:1;10:12; Ufunuo 3:21).

Yeye ndiye ‘’mtu mwenye cheo/kabaila’’ wa mfano, aliyeenda kwenye kiti cha Enzi cha Mungu—‘’nchi ya mbali’’—ali atawezwe kama Mfalme wa wafalme juu ya mataifa na baadaye atarudi duniani (Luka 19:12-27).

Tena, yuko mbinguni hadi ‘’wakati wa kufanywa upya kwa vitu vyote’’ (Matendo 3:19-21). Kuwekwa upya kunamaanisha kuweka vitu kama vile vilivyokuwa zamani. Kwa hali hii, kufanya upya serikali ya Mungu duniani, na baadaye kufanya upya amani ya ulimwengu katika hali kamilifu.

Mtikisiko ulioko ulimwenguni, vita vilivyoenea na migogoro zitafika kileleni katika taabu za ulimwengu kwa njia kubwa sana ambapo Mungu asipoingia kati hakuna mwili wa binadamu utakaookolewa ukiwa hai (Mathayo 24:22). Na katika upeo wake wakati kuchelewa kutakuwepo utasababisha mlipuko wa uhai wote kutoka kwa sayari hii, na Yesu Kristo atarudi. Wakati huu anakuja kama Mungu Mtakatifu. Anakuja katika nguvu zote na utukufu wa mtawala na Muumba wa ulimwengu wote. (Mathayo 24:30;25:31). Anakuja kama

> ‘’Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana’’ (Ufunuo 19:16), kusimamisha serikali kuu na kutawala mataifa yote ‘’na fimbo ya chuma’’ (Ufunuo 19:15;12:5)...
>
> **Kristo Hakukaribishwa?**
>
> Lakini je, wanadamu watashangilia kwa kelele na kumkaribisha yeye kwa upeo wa furaha na shauku---hata makanisa ya kawaida ya Ukristo?
>
> Hawatamkaribisha! Wataamini kwamba yeye ni mpinga Kristo kwa sababu wahudumu wa uongo wa Shetani amewadanganya hivyo (II Wakorintho 11:13-15). Makanisa na mataifa watakasirika kwa kuja kwake (Ufunuo 11:15 na 11:18), na wanajeshi watajaribu kumpiga vita na kumharibu (Ufunuo 17:14)!
>
> Mataifa watajihusisha katika vita vya hali ya hewa vinavyokuja yaani vita vya tatu, na uwanja wa vita utakuwa Yerusalemu (Zekaria 14:1-2) na baadaye Kristo atarudi. Katika nguvu za ajabu ‘’atawapiga vita dhidi ya mataifa’’ ambayo yatajaribu kumpiga (Mstari wa 3). Atawashinda (Ufunuo 17:14)! ‘’Na miguu yake itakanyaga juu mlima wa Mizeituni,’’ unaopatikana upande wa Mashariki wa Yerusalemu (Zekaria 14:4). (Armstrong HW. Mystery of the Ages,1984)

Biblia inaeleza kwamba Yesu atarudi na atashinda, na bado wengi watampiga vita (Ufunuo 19:19). Wengi watadai (kulingana na kukosa kuelewa unabii wa Biblia, lakini pia kwa sababu ya manabii wa uongo na mafumbo) kwamba Yesu anayerudi ni mpinga Kristo wa mwisho!

Yafuatayo pia yanatoka kwa Herbert Armstrong:

> Dini ya kweli-ukweli wa Mungu unaowezeshwa na upendo wa Mungu na kugawiwa na Roho Mtakatifu... FURAHA ISIYO NA

> KIFANI ya kumjua Mungu na Yesu Kristo---ya kujua UKWELI---na furaha ya UPENDO wa Mungu!...
>
> Mafundisho ya Kanisa la Mungu la ukweli ni ''kuishi kwa kila neno'' la Biblia Takatifu...
>
> Wanadamu watageuka kutoka kwa njia ya ''kupokea'' waelekee njia ya ''kutoa''---njia ya upendo wa Mungu. USTARAABU MPYA utakamata dunia! (sawa na hapo)

USTAARABU MPYA ni Ufalme wa Mungu. Kutangaza kwamba ustaarabu mpya utakuja na kujengwa kwenye upendo ni sehemu kubwa ya injili ya ukweli ya ufalme ambayo Yesu na wafuasi wake walifundisha hayo. Na pia ndiyo sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunahubiri pia.

Herbert W. Armstrong aligundua kwamba Yesu alifundisha kuwa jamii za binadamu, hata wakati wanafikiria kutii, wamepuuza ''njia ya maisha ya kutoa'', njia ya upendo. Karibu wote wanaonekana kutoshika na kuelewa umuhimu wa yale aliyofundisha Yesu.

## Wokovu kupitia kwa Yesu ni sehemu ya Injili

Sasa wengine ambao wamesoma hadi hapa pengine wanashangaa kuhusu kufa kwa Yesu na jukumu lake katika wokovu. Ndiyo, hii ndiyo sehemu ya injili ambayo Agano Jipya na Herbert Armstrong aliandika kuhusu.

Agano Jipya linaonyesha kwamba injili ni pamoja na wokovu kupitia Yesu:

> 16 Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia (Warumi 1:16).
>
> 4 Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno. 5 Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria,

akawahubiri Kristo.... [12] Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake. ...[25] Nao walipokwisha kushuhudia na kulihubiri neno la Bwana wakarudi Yerusalemu, wakaihubiri Injili katika vijiji vingi vya Wasamaria.[26] Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. ...[40] Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria. (Matendo 8:4,5,12,25,26,40)

[18] alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufufuo. (Matendo 17:18)

[30] Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea,[31] akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu. (Matendo 28:30-31)

Kumbuka kwamba mafundisho yalikuwa Yesu pamoja NA ufalme. Kwa huzuni, kuelewa kwa ufalme wa Mungu kunaonekana kupotea kutoka kwa mafundisho ya makanisa ya Wagiriki-Rumi.

Kwa hakika, ili Mungu atusaidie tuwe sehemu ya ufalme huo, mungu aliupenda wanadamu sana akatuma Yesu Kristo ili atufie (Yohana 3:16-17).

## Injili ya Ufalme wa Mungu ndiyo Ulimwengu Unahitaji, lakini...

Lakini viongozi wengi pamoja na viongozi wa madhehebu wanaamini ya kwamba utakuwa muungano wa mwanadamu wa kimataifa ambayo yataleta amani na ustawi, na sio Ufalme wa Mungu. Na wakati watakuwa na mafanikio ya muda, na mafanikio haya hayatadumu na juhudi zao za kibinadamu hatimaye italeta uharibifu kiasi kwamba Yesu

asiporudi kusimamisha Ufalme wake, yataharibu kila kitu na wanadamu hawatabaki. Injili yao ni injili ya uongo.

Wengi katika ulimwengu wanajaribu kuzileta pamoja sehemu ya mpango wa kimataifa ya dini ya Babeli ili waweke katika utaratibu mpya wa ulimwengu katika karne ya 21. Hii ndio Kanisa la Mungu Linaloendelea limejaribu kukemea tangu kuanzishwa kwake na linapanga kuendelea kukemea. Tangu Shetani adanganye Hawa ili aanguke katika masimulizi ya injili yake karibia miaka 6000 iliyopita (Mwanzo 3), wanadamu wameamini kwamba wanajua kuliko Mungu chenye kitachowafanya watengeneze ulimwengu uwe mzuri.

Kulingana na Biblia, itakuwa muungano wa kiongozi anayejua vita katika Ulaya (anayeitwa mfalme wa Kaskazini, pia anaitwa mnyama wa Ufunuo 13:1-10) na kiongozi wa dini (anayeitwa nabii wa uongo, pia anaitwa Mpinga Kristo wa mwisho na mnyama mwenye pembe mbili wa Ufunuo 13:11-17) anayetoka kwa mji wa milima saba (Ufunuo 17:9,18) ili walete utaratibu wa ulimwengu wa Kibabeli (Ufunuo 17 na 18). Ingawa mwanadamu anahitaji kurudi kwa Kristo na kuanzishwa kwa Ufalme wake, wengi katika ulimwengu hawatasikia ujumbe huu katika karne ya 21-wataendelea kuamini maelezo mengi ya injili ya uongo ya Shetani. Lakini ulimwengu utapata ushuhuda.

Kumbuka kwamba Yesu alifundisha:

> 14 Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapofika (Mathayo 24:14).

Kumbuka kwamba injili ya ufalme itafika kwa ulimwengu kama ushuhuda ndipo mwisho utafika.

Kuna sababu nyingi zinazofanya injili ifike ulimwenguni kote:

Moja ni kwamba Mungu anataka ulimwengu usikie injili kabla ya Dhiki Kuu haijaanza (ambayo mwanzo wake imeonyeshwa katika Mathayo

24:21). Kwa hivyo ujumbe wa injili ni ushuhuda na onyo (Ezekieli 3, amosi 3:7).

Sababu nyingine ni kwamba kiini cha ujumbe utakuwa kinyume cha mitazamo ya Mnyama anayeinuka, utawala wa Mfalme wa Kaskazini, pamoja na Nabii wa Uongo, mpinga Kristo wa mwisho. Watakuwa wakiahidi amani kupitia kwa juhudi ya wanadamu, lakini itasababisha mwisho (Mathayo 24:14) na uharibifu (1 Wathesalonike 5:3).

Kwa sababu ya ishara na miujiza ya uongo zitakazofuatana nao (2 Wathesalonike 2:9), wengi katika ulimwengu watachagua kuamini uongo (2 Wathesalonike 2:9-12) badala ya ujumbe wa injili. Kwa sababu ya lawama isiyofaa kwa Ufalme wa Mungu wa miaka elfu na Wakatoliki, Othodoksi ya Mashariki, walutheri na wengineo, wengi watadai kimakosa kwamba ujumbe wa injili ya ufalme wa Mungu wa miaka elfu ni injili ya uwongo inayohusiana na Mpinga Kristo.

Wakristo waaminifu wa Filadelfia (Ufunuo 3:7-13) watatangaza injili ya ufalme wa Mungu ya miaka elfu na pia kuwaambia ulimwengu nia ya baadhi ya viongozi wa ulimwengu (pamoja na Mnyama na Nabii wa Uongo).

Watasaidia kuwaambia ulimwengu ujumbe kwamba Mnyama, utawala wa Mnyama wa Kaskazini, pamoja na Nabii wa Uongo, mpinga Kristo wa mwisho, hatimaye ataharibu (pamoja na baadhi ya washirika wake) Marekani na mataifa yanayozungumza Kiingereza ya Uingereza, Canada, australia na Nyuziland (Danieli 11:39) na pia baada ya muda mfupi wataharibu muungano wa Warabu/Waislamu (Danieli 11:40-43), watafanya kama chombo vyombo vya mapepo (Ufunuo 16:13-14), na hatimaye watapigana na Yesu Kristo atakapokuja (Ufunuo 16:14;19:19-20). Wanafiladelfia waaminifu (Ufunuo 3:7-13) watakuwa wakitangaza kwamba ufalme wa miaka elfu umekaribia. Hii itasababisha kunaswa katika vyombo vya habari na itachangia katika utimizaji wa Mathayo 24:14.

Viongozi wa ulimwengu wanaotangaza 'injili ya uwongo' (kama baadhi ya aina ya kiongozi mpya wa cheo cha juu wa Ulaya pamoja na papa mlegevu ambaye ataendeleza aina ya Ukatoliki) hawataipenda injili ya ukweli-hawatapenda ulimwengu wajue watakachofanya (na pia hawataamini injili hiyo (Isaya 10:5-7). Wao na hata wafuasi wao watafundisha kwamba Wanafiladefia waaminifu watakuwa wanashuhudia mafundisho ya kuja kwake mpinga Kristo. Kila lawama ambayo wafuasi wake watatoa dhidi ya Wafiladelfia waaminifu na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) itasababisha mateso (Danieli 11:29-35; Ufunuo 12:13-15). Na hii pia italeta mwisho- yaani mwanzo wa Dhiki Kuu (Mathayo 24:21; Danieli 11:39; mathayo24:14-15; Danieli 11:31) na pia wakati wa ulinzi wa Wakristo Wanafiladelfia waaminifu (Ufunuo 3:10;12:14-16).

Mnyama na Nabii wa Uongo watajaribu kulazimisha, kuleta ulaghai wa uchumi, ishara, miujiza ya uongo, vifo na msukumo (Ufunuo 13:10-17;16:14; Danieli 7:25;2 Wathesalonike 2:9-10) ili wapate kumiliki. Wakristo watauliza:

> 10 Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, ee Mola, mtakatifu, mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipita haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi? (Ufunuo 6:10)

Katika vipindi vyote, watu wa Mungu wamejiuliza, ''Itakuwa hadi lini mpaka Yesu arudi?''

Wakati hatujui siku au saa, tunatarajia Yesu kurudi (na ufalme wa Mungu kuanzishwa) katika karne ya 21 kulingana na maandiko mengi (kv. Mathayo24:4-34; Zaburi 90:4; hosea 6:2; luka 21:7;36; waebrania 1:1-2;4:4;11;2 Petro 3:3-8;1 Wathesalonike 5:4), sehemu zingine ambazo tunaziona zikitimika wakati huu.

Ikiwa Yesu hataingilia kati, ulimwengu utaangamiza uhai wote:

> 21 Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata

sasa, wala haitakuwapo kamwe.[22] Na kama siku hizo zingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo. (Mathayo 24:21-22)

[29] Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika;[30] ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.[31] Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbinguni mpaka mwisho huu. (Mathayo 24:29-31)

Ufalme wa Mungu ndio ulimwengu unahitaji.

## Mabalozi wa Ufalme

Ni nini wajibu wako katika Ufalme?

Sasa hivi, ukiwa Mkristo wa ukweli, unapaswa uwe balozi wa ufalme. Kumbuka alichoandika Mtume Paulo:

[20] Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba Mungu anawasihi kwa kupitia vinywa vyetu, nasi twaomba sana ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu. (2 Wakorintho 5:20)

[14] Kwa hiyo simameni imara mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani,[15] nayo miguu yenu ifungiwe utayari tuupatao kwa Injili ya amani. [16] Zaidi ya hayo, twaeni ngao ya imani, ambayo kwa hayo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. [17] Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. [18] Mkiomba kwa Roho siku zote katika sala zote za maombi,

mkikesha kila wakati mkiwaombea watakatifu wote. [19] Niombeeni na mimi pia, ili kila nifunguapo kinywa changu, nipewe maneno ya kusema, niweze kutangaza siri ya Injili kwa ujasiri,[20] ambayo mimi ni balozi wake katika vifungo. Ombeni ili nipate kuhubiri kwa ujasiri kama inipasavyo. (Waefeso 6:14-20)

Balozi ni nani? Kamusi ya *Merriam-Webster* ina maana zifuatazo:

> 1: mjumbe rasmi; hasa:wakala wa kidiplomasia wa cheo cha juu anaye vibali vya serikali vya kigeni ama mtawala kama mkaaji mwakilishi wa serikali yake ama mtu huru au amechaguliwa kwa njia ya kipekee na mara nyingi kwa shughuli za kidiplomasia za muda.
>
> 2. Mwakilishi aliyeidhinishwa ama mjumbe.

Ikiwa wewe ni Mkristo wa ukweli, wewe ni mjumbe rasmi wa Kristo! Tazama aliyoandika Mtume Petro:

> [9] Lakini ninyi ni taifa teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu la Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa zake yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu. [10] Mwanzo ninyi mlikuwa si taifa, lakini sasa ninyi ni taifa la Mungu. Mwanzo mlikuwa hamkupata rehema, lakini sasa mmepata rehema. ( 1 Petro 2:9-10)

Kama Wakristo, tunafaa tuwe sehemu ya taifa takatifu.

Taifa gani ni takatifu sasa hivi?

Hamna ufalme ambao ni takatifu katika ulimwengu huu-lakini hatimaye watakuwa sehemu ya ufalme wa Kristo (Ufunuo 11:15). Taifa la Mungu ndilo takatifu.

Kama mabalozi, hatufai kushiriki katika siasa ya hadharani ya mataifa ya ulimwengu huu. Lakini tunatakikana tuishi kwa njia ya Mungu sasa.

Kwa kufanya hivyo, tunatakikana tujifunze kuwa njia ya Mungu ndiyo muhimu sana, ili kwamba katika ufalme tuwe wafalme na makuhani na kutawala na Kristo hapa duniani:

> [5] Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,[6] na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu; Utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina. (Ufunuo 1:5-6)

> [10] Wewe umewafanya hawa wawe ufalme na makuhani wa kumtumikia Mungu wetu, nao watatawala duniani. (Ufunuo 5:10 Neno Biblia)

Kipengele kimoja cha wakati ujao ni kwamba tutafundisha wale ambao wana mwili wa binadamu wakati huo katika njia za Mungu:

> [19] Kwa maana watu watakaa katika Sayuni huko Yerusalemu; wewe hutalia tena; hakika yake atakuonea rehema nyingi kwa sauti ya kilio chako; asikiapo ndipo atakapokujibu.[20] Na ingawa Bwana atawapeni chakula cha shida na maji ya msiba, lakini walimu wako hawatafichwa tena, ila macho yako yatawaona waalimu wako;[21] na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, njia ni hii ifuateni mgeukapo kwenda mkono wa kushoto. (Isaya 30:19-21)

Wakati yaliyoandikwa hapo juu ni unabii unaoashiria ufalme wa miaka elfu, katika kipindi hiki, wakristo wanapaswa kujiandaa kufundisha:

> [12]... Kwa maana iwapasayo kuwa waalimu (Waebrania 5:12)

> [15] Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu (1 Petro 5:15).

Biblia inaonyesha kwamba wengi wa Wakristo walio waaminifu sana watafundisha wengi sana kabla ya Dhiki Kuu:

[33] Na hao walio wenye hekima katika watu watafundisha wengi (Danieli 11:33).

Kwa hivyo, kujifundisha, kukua katika neema na kumjua Bwana (2 Petro 3:18), ni kazi ambayo tunafaa tufanye sasa. Sehemu ya jukumu katika Ufalme wa Mungu ni kuweza kufundisha. Na kwa Wakristo Wanafiladelfia waaminifu sana (Ufunuo 3:7-13), hii pia itakuwa pamoja na kusaidia injili ya mshahidi kabla ya ufalme wa miaka elfu kuanzishwa (Mathayo 24:14).

Baada ya Ufalme wa Mungu kuanzishwa, watu wa Mungu watatumika kurekebisha sayari iliyoharibika:

> [12] Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; Utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, mwenye kurejeza njia za kukalia. (Isaya 58:12)

Kwa hivyo watu wa Mungu walioishi katika njia za Mungu watawezesha watu kuishi katika miji (na sehemu zingine) wakati wa kuweka vitu sawa. Ulimwengu kwa ukweli utakuwa mahali pazuri. Tunapaswa tuwe mabalozi wa Kristo sasa, ili kwamba tutawale katika Ufalme wake.

## Ujumbe wa Injili ya Kweli Inageuza

Yesu alisema, ‘’31 Ninyi mkikaa katika Neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli;32 tena mtaifahamu kweli, nayo iyo kweli itawaweka huru.’’ (Yohana 8:31-32). Kujua ukweli kuhusu ufalme wa Mungu utatuweka huru kutoka kwa mafungo ya matumaini ya uwongo ya ulimwengu huu. Tunaweza kuunga mkono mpango unaofanya kazi-mpango wa Mungu! Shetani ameudanyanyanya ulimwengu mzima (Ufunuo 12:9) na Ufalme wa Mungu ndio suluhisho. Tunafaa tusimame kwa ukweli na kutetea ukweli (Yohana 18:37).

Ujumbe wa injili ni zaidi ya wokovu wa kibinafsi. Habari njema ya Ufalme wa Mungu inapaswa kugeuza mtu katika kipindi hiki:

> [2] Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu. (Warumi 12:2)

Wakristo wa ukweli wamegeuzwa kutumikia Mungu na wengine:

> [22] Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana.[23] Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa moyo kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu,[24] mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo. (Wakosolai 3:22-24)

> [28] Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho. (Waebrania 12:28)

Wakristo wa ukweli wanaishi tofauti na ulimwengu. Tunakubali vipimo vya Mungu kwa kile kibaya na chema kuliko kutumia vya ulimwengu. Wenye haki wataishi kwa imani (Waebrania 10:38), kwa sababu inahitaji imani ili uishi katika njia ya Mungu siku hizi. Wakristo walichukuliwa kuwa tofauti sana na ulimwengu walimoishi kiasi kwamba njia ya maisha yao waliitwa ‘’Watu wa Njia’’ katika Agano Jipya (Matendo 9:2;19:9;24:14,22). Ulimwengu unaishi kiubinafsi, Chini ya utawala wa Shetani, kwa kile kinachoitwa ‘’njia ya Kaini’’(Yuda 11).

Injili ya Ufalme wa Mungu ni ujumbe wa haki, furaha na amani (Warumi 14:17). Neno la unabii, likifahamika vizuri lafariji (1 Wakorintho 14:3;1 Wathesalonike 4:18), haswa tukiona ulimwengu ukibomoka (Luka 21:8-36). Njia ya ukweli ya maisha ya Ukristo

inaongoza kwenye wingi wa kiroho na baraka za kimwili (Marko 10:29-30). Hii ndiyo maana wanaoishi kwa kutarajia ufalme wanaelewa kwamba ulimwengu unahitaji Ufalme wa Mungu. Wakristo ni mabalozi wa Ufalme wa Mungu.

Wakristo wanaweka matumaini yao katika mambo ya kiroho siyo ya kimwili, hata hivyo tunaishi katika ulimwengu (Warumi 8:5-8). Tunalo ''tumaini la injili'' (Wakolosai 1:23). Hili ni jambo ambalo Wakristo wa awali walielewa ambalo wengi wanaokiri kuwa Wakristo leo hii hawafahamu.

# 6. Makanisa ya Wagiriki-Warumi Wanafundisha Kwamba Ufalme ni wa Muhimu, lakini...

Makanisa ya Wagiriki-Warumi wanaamini kwamba wanafundisha baadhi ya dhana ya Ufalme wa Mungu, lakini wana shida ya kufahamu uhakika wake. Kwa mfano kamusi elezo ya Katoliki inafundisha yafuatayo kuhusu ufalme:

> Kristo... Katika awamu ya kufundisha kuja kwa ufalme huu, vipengele vyake mbalimbali, maana yake halisi, vile mtu anaweza kuufikia ufalme ndilo lilikuwa wazo kuu la mahubiri yake, kiasi kwamba mahubiri yake yanaitwa ‘’injili ya ufalme’’... Wakaanza kuliita kanisa kama ‘’ufalme wa Mungu,’’ Wakolosai I,13; I Wathesalonike., ii,12; apok., i,6,9;v,10, nk. ... Inamaanisha kanisa kama taasisi ya kimungu... (Pope H. Kingdom of God. The Catholic Encyclopedia, volume VIII. 1910).

Hata hivyo yaliyo juu yanaashiria ‘’Wakolosai.,1,13;I Wathesalonike., ii,12; apok., i,6,9;v,10,’’ ukiyatazama maandiko haya utapata kwamba hakuna linalotaja kanisa kama Ufalme wa Mungu. Yanafundisha kwamba waaminio watakuwa katika Ufalme wa Mungu ama kwamba ni Ufalme wa Kristo. Biblia inaonya kwamba wengi watabadilisha injili na kugeukia injili nyingine, injili ya uwongo (Wagalatia 1:6-9). Kwa huzuni, wengi wamefanya hivyo.

Yesu alifundisha, ‘’Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi (Yohana 14:6). Paulo alifundisha, ‘’Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo’’ (Matendo 4:12). Petro aliwaambia Wayahudi kwamba wote lazima wawe na imani ya kutubu na kumkubali Yesu ili waokolewe(Matendo 2:38).

Kwa kutofautisha haya, papa Francis amefundisha kwamba wakafiri, bila Yesu wanaweza kuokolewa kwa kazi nzuri!Pia anafundisha kwamba Wayahudi wanaweza kuokolewa bila kumkubali Yesu! Zaidi ya hayo, yeye na baadhi ya Wagiriki-Warumi pia wanasema kwamba maelezo yasiyo ya kibiblia ya 'Maria' pia ni msingi wa injili na pia ni msingi wa muungano wa ekumeni na wa madhehebu. Kwa huzuni wao na wengine hawaelewi umuhimu wa Yesu NA Injili ya ukweli ya Ufalme wa Mungu. Wengi wanaendeleza injili ya uwongo.

Wengi wanataka kutembea kwa kuona na wana imani katika ulimwengu. Agano Jipya linafundisha kwamba Wakristo wanapaswa kutazama yaliyo juu:

> 2 Yafikirini yaliyo juu, sio yaliyo katika nchi. (Wakolosai 3:2)
>
> 7 Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona. (2 Wakorintho 5:7)

Ijapokuwa, papa Pius alifundisha kutembea kwa kuona kwa kutumia kanisa lake:

> ... Kanisa la Katoliki... Ndio Ufalme wa Mungu katika dunia. (Pius's encyclical Quas Primas as cited in Kramer P. The Devil's Final Battle.Good Counsel Publications,2002, p.73).

Tovuti ya *catholicBible101* inadai kwamba, ''Ufalme wa Mungu ulianzishwa duniani na Yesu Kristo mnamo mwaka wa 33 B. K, kwa Kanisa lake, likiongozwa na Petro..., yaani Kanisa la Katoliki.'' Lakini Ufalme wa Mungu wa miaka elfu haupo hapa wala sio kanisa la Rumi, lakini utakuwa duniani.

Kanisa la Rumi linafundisha kwa nguvu dhidi ya Ufalme wa Mungu ambao utakuja hivi karibuni hapa duniani wa miaka elfu kwamba hilo pekee ndilo ''fundisho la Mpinga Kristo'' ambalo limepangwa katika *Katekismo rasmi ya Kanisa la Katoliki*.

> [676] Uwongo wa Mpinga Kristo tayari umeanza kuchukua umbo katika ulimwengu huu wakati wo wote madai yanafanywa kugundua ndani ya historia kwamba tumaini la Masihi ambalo laweza kugunduliwa zaidi ya historia kupitia kwa hukumu ya mwisho. Kanisa limepuuzia hata aina ya marekebisho ya uwongo wa ufalme wa ulimwengu unaokuja chini ya jina la milenia... (Catechism of the Catholic Church. Imprimatur Potest+Joseph Cardinal Ratzinger). Doubleday, nY 1995, p. 194)

Kwa huzuni, wanaokubaliana na hayo watakuwa na shida kubwa na kutangaza Injili ya Ufalme wa Mungu katika nyakati za mwisho. Baadhi yao watachukua hatua ya hatari dhidi ya wale watakaotangaza Injili hiyo (Danieli 7:25;11:30-36).

Lakini, unaweza kufikiria kama wote wanaokiri Kristo kama Bwana watakuwa katika ufalme? Hapana, hawatakuwamo. Kumbuka alichosema Yesu:

> [21] Si kila mtu aniambiaye, bwana, bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.[22] Wengi wataniambia siku ile, bwana, bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? [23] Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. (Mathayo 7:21-23)

Mtume Paulo aligundua ''siri ya uasi'' ilikuwa ''inatenda kazi'' (2 Wathesalonike 2:7) katika wakati wake. Uasi huu pia unahusiana na kitu ambacho Biblia inaonya dhidi yake katika nyakati za mwisho ambacho kinaitwa ''Siri, babeli Mkuu'' (Ufunuo 17:3-5).

''Siri ya uasi'' inahusiana na wanaokiri Kristo ambao wanaamini kwamba hawana haja na kufuata Amri kumi za Mungu n. K na/ama kuna baadhi ya ubaguzi kwa amri na/ama kuna aina ya makubaliano ya toba ya kuvunja amri ya Mungu, basi wakati wanafikiri kwamba hiyo ni

aina ya amri ya Mungu, hawatunzi aina ya ukristo ambao Yesu na mitume wake wangethamini kuwa halali.

Wagiriki-Warumi ni kama Mafarisayo ambao walikiuka amri za Mungu, lakini walitangaza mapokeo yao na kuyafanya watu kukubaliana nayo- Yesu alilaani mbinu hiyo (Mathayo 15:3-9)! Isaya pia alionya kwamba watu wanaodai kuwa ni wa Mungu wataasi dhidi ya amri yake (Isaya 30:9). Uasi wa sheria ndio tunaona ukifanyika hadi leo.

''Siri'' ingine inaonekana kwamba Kanisa la Rumi linaonekana kuamini kwamba umoja wa dini na ajenda ya muungano wa kivita zitaongoza kwa amani na aina ya Ufalme wa Mungu wa dunia isiyo ya kibiblia. Maandiko yanaonya dhidi ya umoja wa madhehbu ambao Biblia inafundisha kufanikiwa kwa miaka michache (note:the *New Jerusalem Bible*, a Catholic-approved translation, is shown):

> 4 Watu wakaliabudu lile joka kwa sababu lilikuwa limempa huyo mnyama mamlaka yake, pia wakamwabudu huyo mnyama na kuuliza, ''Ni nani aliye kama huyu mnyama? Ni nani awezaye kupigana vita naye?'' 5 Huyo mnyama akapewa kusema maneno ya kujisifu na kukufuru na kutumia mamlaka yake kwa muda wa miezi arobaini na miwili. 6 Akafungua kinywa chake ili kumkufuru Mungu, akilitukana jina lake na mahali aishipo na wale wakaao mbinguni. 7 Pia akaruhusiwa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda. Akapewa uwezo juu ya kila kabila, jamaa, lugha na taifa. 8 Nao watu wote waishio duniani watamwabudu huyo mnyama, yaani wale wote ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu. 9 Yeye aliye na sikio na asikie. 10 Ikiwa mtu ni wa kuchukuliwa mateka, atachukuliwa mateka. Ikiwa mtu ni wa kuuawa kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye wito kwa ajili ya saburi na imani ya watakatifu. (Ufunuo 13:4-10, nJB)

Biblia huonya dhidi ya muungano wa nyakati za mwisho wa kibabeli:

1 Mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na yale mabakuli
saba akaja akaniambia, ''Njoo, nitakuonyesha adhabu ya yule
kahaba mkuu, aketiye juu ya maji mengi. 2 Yule ambaye
wafalme wa dunia walizini naye na watu wakaao duniani
walilewa kwa mvinyo wa uzinzi wake.'' 3 kisha yule malaika
akanichukua katika Roho akanipeleka nyikani. Huko
nikamwona mwanamke mmoja ameketi juu ya mnyama
mwekundu aliyejaa majina ya kumkufuru Mungu mwili mzima.
Mnyama huyo alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. 4 Huyo
mwanamke alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya zambarau na
nyekundu, akimetameta kwa dhahabu, viti vya thamani na
lulu. Mkononi mwake alikuwa ameshika kikombe cha dhahabu
kilichojaa mambo ya machukizo na uchafu wa uzinzi wake. 5
Kwenye kipaji chake cha uso palikuwa pameandikwa jina:

''SIRI, bABELI MKUU, mAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO
YA DUNIA.'' 6. Nikaona kuwa huyo mwanamke alikuwa
amelewa kwa damu ya watakatifu, yaani damu ya wale watu
waliouawa kwa ushuhuda wa Yesu. (Ufunuo 17:1-6, nJB)

9 ''Hapa ndipo penye akili pamoja na hekima. Vile vichwa saba
ni vilima saba ambavyo huyo mwanamke amevikalia... 18 Yule
mwanamke uliyemwona ni ule mji mkubwa unaotawala juu ya
wafalme wa dunia.'' (Ufunuo 17:9,18, nJB)

1 Baada ya haya nikaona malaika mwingine akishuka kutoka
mbinguni, akiwa na mamlaka makuu na dunia ikamulikiwa na
mng'ao wake. 2 Naye akalia kwa nguvu kwa sauti kubwa,
akisema: ''Umeanguka! Umeangika Babeli uliye Mkuu!
Umekuwa makao ya mashetani na makazi ya kila pepo mchafu,
makazi ya kila ndege na kila mnyama achukizaye. 3 Kwa maana
mataifa yote yamekunywa mvinyo wa uasherati wake. Nao
wafalme wa dunia wamefanya biashara wa dunia wametajirika
kutokana na wingi wa utajiri wake.'' 4 Kisha nikasikia sauti
nyingine kutoka mbinguni ikisema: ''Tokeni katikati yake, enyi
watu wangu, ili msije mkashiriki dhambi zake, ili msije

mkapatwa na pigo lake lo lote;[5] kwa kuwa dhambi zake zimerundikana hadi mbinguni, naye Mungu ameukumbuka uhalifu wake.[6] Mtendee kama yeye alivyotenda; Umlipe mara mbili kwa ajili ya yale aliyotenda. Katika kikombe chake mchanganyie mara mbili ya kile alichochanganya.[7] Mpatie mateso na huzuni nyingi sawa na utukufu na anasa alizojipatia. Kwa kuwa moyoni mwake hujivuna, akisema, mimi ninatawala kama malkia; mimi si mjane, wala sitaona huzuni kamwe.' [8.] Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku moja:mauti maombolezo na njaa. Naye atateketezwa kwa moto, kwa maana amhukumuye ni BWANA Mungu Mwenyezi.[9] ''Wafalme wa dunia waliozini naye na kushiriki anasa zake watakapoona moshi wa kuungua kwake, watamlilia na kumwomboleza. (Ufunuo 18:1-9 NJB)

Katika Zekaria, biblia inaonya dhidi ya Babeli inayokuja na inaonyesha kwamba umoja unaofaa hautakuwepo hadi Yesu arudi:

[6] Haya! Haya! Ikimbieni nchi ya kaskazini, asema BWANA; kwa maana mimi nimewatawanya ninyi kama pepo nne za mbinguni, asema BWANA.[7] Haya! Ee Sayuni, jiponye, wewe ukaaye pamoja na binti Babeli.[8] Kwa maana BWANA wa majeshi asema hivi, ili nitafute utukufu umenituma kwa mataifa wale waliowateka ninyi; maana yeye awagusaye ninyi aigusa mboni ya jicho lake.[9] Kwa maana, tazama, nitatikisa mkono wangu juu yao, nao watakuwa mateka ya hao waliowatumikia; nanyi mtajua ya kuwa BWANA wa majeshi amenituma. [10] Imba, ufurahi, ee Binti Sayuni; maana, tazama ninakuja, nami, nitakaa kati yako, asema BWANA. [11] Na mataifa mengi watajiunga na BWANA katika siku ile, nao watakuwa watu wangu; nami nitakaa kati yako, nawe utajua ya kuwa BWANA wa majeshi amenituma kwako. [12] Na BWANA atairithi Yuda, iwe sehemu yake katika nchi takatifu, naye atachagua Yerusalemu tena. (Zekaria 2:6-12)

Harakati ya muungano wa madhehebu na umoja wa makanisa ambao viongozi wa Muungano wa Mataifa, vatikani, waprotestani wengi na Othodoksi wa Mashariki wanaendeleza umelaaniwa na Biblia na haupaswi kuhamasishwa. Yesu alionya dhidi ya atakayejidai kumfuata na huku ‘’akiwadanganya wengi’’ (Mathayo 24:4-5). Muungano wa madhehebu unahusiana na ‘’farasi mweupe’’ wa Ufunuo 6:1-2 (ambaye SI Yesu) na kahaba wa Ufunuo 17.

Kama Zekaria, mtume Paulo pia alifundisha kwamba umoja wa imani hautafanyika hadi Yesu arudi:

> [13] mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima kwa kufikia kimo cha ukamilifu wa Kristo. (Waefeso 4:13, nJB)

Wale wanaoamini kwamba umoja huu unakuja kabla ya Yesu kurudi wako katika upotofu. Kwa hakika, yesu akirudi, ataharibu umoja wa mataifa ambao wataungana kumpiga vita:

> [15] Yule malaika wa saba akapiga tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni iliyosema: ‘’Ufalme wa ulimwengu umekuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala milele na milele.’’ [16] Nao wale wazee ishirini na wane, aliokuwa wameketi mbele za Mungu, kwenye viti vyao vya enzi wakaanguka kifudifudi wakamwabudu Mungu,[17] wakisema: ‘’Tunakushukuru, bWANA Mungu Mwenyezi, uliyeko na uliyekuwako, kwa kuwa umetwaa uweza wako mkuu na ukaanza kutawala. [18] Mataifa walikasirika kwa kuwa wakati wa ghadhabu Yako umewadia wa kuwahukumu waliokufa na kuwapa thawabu watumishi wako manabii na watakatifu wako pamoja na wale wote wanaoliheshimu Jina Lako, wakubwa kwa wadogo:na kuwaangamiza wale wanaoiangamiza dunia.’’ (Ufunuo 11:15-18, nJB)

> [6] Kisha nikasikia sauti kama ya umati mkubwa, kama sauti ya maji mengi yaendayo kasi na kama ngurumo kubwa ya radi

> wakipiga kelele wakisema: ''Haleluya! Kwa maana BWANA Mungu wetu Mwenyezi anatawala. [19] Kisha nikamwona yule mnyama na wafalme wa dunia pamoja na majeshi yao wakiwa wamekusanyika pamoja ili kufanya vita dhidi ya yule aliyempanda huyo farasi mweupe pamoja na jeshi lake.[20] Lakini yule mnyama akakamatwa pamoja na huyo nabii wa uongo ambaye alikuwa amefanya ishara kwa niaba ya huyo mnyama, ambaye kwa ishara hizi aliwadanganya wale waliopokea chapa ya huyo mnyama na kuiabudu sanamu yake. Hawa wawili wakatupwa wakiwa hai ndani ya ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti.[21] Wale waliosalia waliuawa kwa upanga uliotoka kinywani mwa yule aliyekuwa amempanda huyo farasi mweupe, nao ndege wote wakajishibisha kwa nyama yao. ...[20:4]Kisha nikaona viti vya enzi vilivyokuwa vimekaliwa na hao waliopewa mamlaka ya kuhukumu. Nami nikaona roho za wale waliokatwa vichwa kwa sababu ya ushuhuda wa Yesu na kwa sababu ya neno la Mungu. Hawakuwa wamemsujudu huyo mnyama wala sanamu yake wala hawakupokea ile chapa yake kwenye vipaji vya nyuso zao au kwenye mikono yao. Wakawa hai na kutawala pamoja na Kristo miaka 1,000. (Ufunuo 19:6,19-21;20:4, nJB)

Kumbuka kwamba Yesu lazima ataharibu majeshi ya ulimwengu ambao wameungana dhidi yake. Alafu yeye na watakatifu wake watatawala. Hapo ndipo kutakuwako na umoja kamili ya imani.

Kwa huzuni, wengi watawasikiliza wahudumu waongo ambao wanaonekana wazuri, lakini sio kama vile Mtume Paulo anavyoonya (2 Wakorintho 11:14-15).

Ikiwa wengi wangeelewa ukweli wa Biblia na injili ya Ufalme wa Mungu wachache wangepiga vita dhidi ya Yesu.

# 7. Kwa Nini Ufalme wa Mungu?

Hata kama wanadamu wanafikiri ni werevu sana, kuna kiwango cha kuelewa kwetu, lakini ''akili za Mungu hazina mpaka'' (Zaburi 147:5).

Ndiyo maana itachukua kuingilia kati kwa Mungu ili aweke sayari hii sawa.

Wakati wengi wanaamini katika Mungu, wengi wa wanadamu hawako tayari kuishi kama vile anatuongoza. Kumbuka yafuatayo:

> 8 Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na BWANA anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! (Mika 6:8)

Kwenda kwa unyenyekevu na Mungu ni kitu ambacho mwanadamu hajakuwa na nia ya kufanya. Kuanzia wakati wa Adamu na Hawa (Mwanzo 3:1-6), wanadamu wamechagua kujitegemea peke yao na vipaumbele vyao, bila Mungu, bila kutunza amri zake (Kutoka 20:3-17).

Kitabu cha Mithali kinafundisha:

> 5 Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; 6 Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako. 7 Usiwe mwenye hekima machoni pako; mche BWANA, ukajiepushe na uovu. (Mithali 3:5-7)

Na bado wengi hawatamtumaini Mungu na mioyo yao yote ama kumngoja awaelekeze hatua zao. Wengi wanasema watafanya anachohitaji Mungu, lakini hawafanyi. Mwanadamu amedanganywa na Shetani (Ufunuo 12:9) na wameanguka kwa tamaa za ulimwengu na ‘kiburi cha uzima’ (1 Yohana 2:16).

Kwa hivyo, wengi wamekuja na mapokeo yao ya dini na serikali ya kawaida, kwa sababu wanafikiri wanajua zaidi. Hata hivyo, hawajui (Yeremia 10:23) na hata wengi hawatatubu.

Hiyo ndiyo maana wanadamu wanahitaji Ufalme wa Mungu (Mathayo 24:21-22).

## Njia za Mungu ni za Haki

Ukweli ni kwamba Mungu ni upendo (1 Yohana 4:8,16) na Mungu sio mbinafsi. Amri za Mungu zaonyesha upendo kwa Mungu na jirani (Marko 12:29-31; jakobo 2:8-11). Njia za ulimwengu ni za ubinafsi na zinaelekea mautini (Warumi 8:6).

Kumbuka kwamba Biblia inaonyesha kwamba Wakristo wa ukweli walitunza amri:

> 1 Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye.2 Katika hili twajua kwamba twapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huko ndiko kumpenda Mungu kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito. (1 Yohana 5:1-3)

Amri za Mungu zote ni za haki (Zaburi 119:172). Njia zake ni safi (1 Timotheo 1:5). Kinachohuzunisha ni kwamba wengi wamekubali aina za ''maasi'' na hawagundui kwamba Yesu HAKUJA kuharibu amri au manabii, lakini kuzitimiliza (Mathayo 5:17), kwa kueleza maana zao na kupanua zaidi ya waliyokuwa wamejua (k. V. Mathayo 5:21-27). Yesu alifundisha kwamba, ''bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.'' (Mathayo 5:19) (Neno Ufalme wa Mungu na Ufalme wa mbinguni yanafanana).

Biblia inafundisha kwamba imani bila matendo imekufa (Yakobo 2:17). Wengi wanadai kwamba wanafuata Yesu, lakini kwa kweli hawataamini mafundisho yake (Mathayo 7:21-23) na hawatamuiga kama inavyotakikana (1 Wakorintho 11:1).''Dhambi ni kuasi sheria'' (1 Yohana 3:4) na wote wametenda dhambi(Warumi 3:23). Hata hivyo, biblia inaonyesha kwamba huruma hujitukuza juu ya hukumu (Yakobo 2:13) kwa sababu Mungu ana mpango kwa wote (Luka 3:6).

Suluhisho la mwanadamu bila njia ya Mungu halitafanya kazi. Katika utawala wa miaka elfu, yesu atatawala na ''fimbo ya chuma'' (Ufunuo 19:15), na mema utafaulu kwa sababu watu wataishi katika njia za Mungu. S**hida ZOTE za ulimwengu zimekuwepo kwa sababu jamii za ulimwengu huu wamekataa kumtii Mungu na Amri zake**. Historia inaonyesha kwamba wanadamu hawawezi kusuluhisha shida za jamii:

> [6] Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani.[7] Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.[8] Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. (Warumi 8:6-8)

Wakristo wanapaswa kuzingatia mambo ya kiroho, na wapewe Roho wa Mungu ili wafanye hivyo katika nyakati hizi (Warumi 8:9), licha ya udhaifu wetu:

> [26] Maana, maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa;[27] bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu;[28] tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; [29] mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu.[30] Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;[31] kusudi, kama ilivyoandikwa, yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana. (1 Wakorintho 26-31)

Wakristo wanapaswa kutukuza katika mpango wa Mungu! Tunatembea kwa imani sasa (2 Wakorintho 5:7), wakiangalia yaliyo juu (Wakolosai 3:2) katika imani (Waebrania 11:6). Tutabarikiwa kwa kutunza amri za Mungu (Ufunuo 22:14).

Biblia inasema kwamba Wakristo watatawala na Yesu, lakini je, unagundua kwamba watatawala juu ya miji? Yesu alifundisha:

> [12] Basi akasema, mtu mmoja, kabaila, alisafiri kwenda nchi ya mbali, ili ajipatie ufalme na kurudi. [13] Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, fanyeni biashara hata nitakapokuja. [14] Lakini watu wa mji wake walimchukia, wakatuma wajumbe kumfuata na kusema, hatumtaki huyu atutawale. [15] Ikawa aliporudi, ameupata ufalme wake, aliamuru waitwe wale watumwa aliowapa fedha, ili ajue faida aliyopata kila mtu kwa biashara yake. [16] Akaja wa kwanza, akasema, bwana fungu lako limeleta faida ya mafungu kumi zaidi. [17] Akamwambia, vema, mtu mwema; kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo, uwe na mamlaka juu ya miji kumi. [18] Akaja wa pili, akasema, bwana, fungu lako limeleta mafungu matano faida. [19] Akamwambia huyu naye, wewe uwe juu ya miji mitano. (Luka 19:12-19)

Uwe mwaminifu juu ya mambo madogo unayo sasa. Wakristo watakuwa na nafasi ya kutawala juu ya miji halisi, katika ufalme halisi. Yesu pia alisema, ''Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo'' (Ufunuo 22:12). Mungu ana mpango (Ayubu 14:15) na mahali (Yohana 14:2) pa wale watakaoitikia wito wake (Yohana 6:44; Ufunuo 17:14). Ufalme wa Mungu ni halisi na unatakikana uwe sehemu katika ufalme huo!

Mwanzo wa 2016, jarida la Sayansi lilikuwa na makala iitwayo ''nguvu ya umati'' ambayo ilionyesha kwamba akili ya bandia na chanzo cha umati vinaweza kusuluhisha 'shida za maovu' ambazo zinakabiliana na wanadamu. Na bado, makala hii ilikosa kufahamu maana ya uovu, mbali na hata kusuluhisha.

Ushirikiano, mbali na kuzifuata njia za kweli za Mungu, hauwezi kufaulu katika karne ya 21 kama vile ilivyokuwa baada ya Gharika

Kubwa wakati wanadamu walishirikiana na kujenga Mnara wa Babeli ulioanguka (Mwanzo 11:1-9).

Matatizo katika ulimwengu, katika maeneo kama Mashariki ya Kati (licha ya faida zisizodumu k. V. Danieli 9:27a,1 Wathesalonike 5:3), hayatasuluhishwa na wanadamu-twahitaji amani ya Ufalme wa Mungu (Warumi 14:17).

Shida za ugaidi wa kimataifa, licha ya faida zinazotarajiwa, hazitasuluhishwa (Ezekieli 21:12) na wanaodanganywa katika Umoja wa Mataifa (Ufunuo 12:9)-twahitaji furaha na faraja ya Ufalme wa Mungu.

Shida za mazingira hazitasuluhishwa na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa sababu mataifa ya ulimwengu watasaidia kuharibu dunia (Ufunuo 11:18), lakini zitasuluhishwa na Ufalme wa Mungu.

Shida za usinzi, utoaji mimba na kuuza sehemu za mwili wa mwanadamu na Marekani hazitasuluhishwa na mwanadamu lakini na Ufalme wa Mungu.

Deni kubwa ambazo Marekani, uingereza na mataifa mengi wanazo hazitasuluhishwa kupitia kwa wakala wa kimataifa, lakini mwishowe (baada ya uharibifu kulingana na Habakuki 2:6-8) na Ufalme wa Mungu.

Ujinga na kukosa elimu hazitasuluhishwa na Umoja wa Mataifa-twahitaji Ufalme wa Mungu. Ugomvi wa dini hautasuluhishwa na harakati ya muungano wa madhehebu unaokubaliana na wokovu bila Yesu wa ukweli wa Biblia). Dhambi ndiyo SHIDA katika ulimwengu na kwa hivyo, twahitaji kutolewa sadaka kwa Yesu na kurudi kwake katika Ufalme wa Mungu.

Masuala ya njaa hayatasuluhishwa na mazao yenye vinasaba ambayo yanaweka ulimwengu katika hatari ya njaa kwa sababu ya mimea kutofaulu-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Sayansi ya matibabu ya kisasa haina majawabu yote ya afya ya wanadamu-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Umaskini kubwa katika katika sehemu za Afrika, asia na sehemu zingine, wakati watafaulu kidogo kwa muda kutoka kwa Babeli wa siku za mwisho (Ufunuo 18:1-19), hazitasuluhisha shida za umaskini-twahitaji Ufalme wa Mungu.

Awamu ya miaka elfu ya Ufalme wa Mungu ni ufalme halisi ambao utasimamishwa duniani. Utajengwa juu ya sheria za upendo wa Mungu na Mungu mwenye upendo kama kiongozi. Watakatifu watatawala na Kristo kwa miaka elfu (Ufunuo 5:10;20:4-6). Huu Ufalme utakuwa na watu ambao kwa ukweli wako katika Kanisa la Mungu, lakini hakuna maandiko yanayoeleza ya kwamba Kanisa ni Ufalme (Ya kikatoliki ama maandiko mengine). Kanisa la Rumi wamepinga mafundisho ya ufalme wa miaka elfu, na baadaye litapinga kwa nguvu ujumbe wa injili ya Biblia tukikaribia kufika mwisho. Na hii itavuta sana vyombo vya habari ambayo itasaidia kutimiza Mathayo 24:14.

Katika awamu yake ya mwisho, ufalme wa Mungu utajumuisha ''Yerusalemu mpya , ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu'' (Ufunuo 21:2) na katika maongeo yake hayatakuwa na mwisho. Hakutakuwepo na udhalimu tena na huzuni na mauti tena.

Kuhubiri na kuelewa injili ya Ufalme wa Mungu ndiyo mada kuu ya Biblia. Waandishi wa Agano la Kale walifundisha injili hiyo. Yesu, paulo na Yohana walifundisha injili hiyo.

Mahubiri ya kale yaliyo nje ya Agano Jipya yalifundisha ufalme. Viongozi wa awali wa karne za kwanza kama Polycarp na Melito, walifundisha injili hii. Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunafundisha injili hii leo.

Kumbuka kwamba Ufalme wa Mungu ndio somo la kwanza ambalo Biblia ilionyesha Yesu alifundisha. Na ndiyo injili Yesu alifundisha baada ya ufufuo-na ni kitu Wakristo wanapaswa kuutafuta kwanza.

Injili haihusu maisha na kifo pekee ya Yesu. Msisitizo wa injili ambao Yesu na wanafunzi wake walifundisha ulikuwa ni Ufalme wa Mungu unaokuja. Injili ya ufalme inabeba wokovu kupitia kwa Kristo, na pia inahusu mafundisho ya mwisho wa serikali za wanadamu (Ufunuo 11:15).

Kumbuka Yesu alifundisha kwamba mwisho hautafika mpaka injili ya Ufalme wa Mungu uhubiriwe ulimwenguni kama ushuhuda kwa mataifa yote (Mathayo 24:14). Na mahaubiri yanaendelea sasa.

Habari njema ni kwamba **Ufalme wa Mungu ndio suluhisho la shida zinazokabili wanadamu**. Ijapokuwa wengi hawataki kukubali, kusikia na hata kuamini ukweli wake. Ufalme wa Mungu ni wa milele (Mathayo 6:13), wakati ''ulimwengu huu unapita'' (1 Wakorintho 7:31).

Kutangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu ndiko tunafanya kwa bidii katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG). Tunajitahidi kufundisha mambo yote ambayo Biblia inafundisha (Mathayo 28:19-20), pamoja na Ufalme wa Mungu (Mathayo 24:14). Wakati tunaungoja Ufalme, twahitaji kujifunza na kuzifuata njia za Mungu na kufariji wengine ambao wanataka kuamini ukweli.

Je, utaunga mkono kutangaza kwa injili ya kurudi kwa Ufalme wa Mungu? Je utaamini injili ya Ufalme wa Mungu?

# Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)

**Afisi ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) inapatikana**:1036 W.Grand Avenue, Grover Beach, California,93433 USA.
**Tovuti za Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)**

**CCOG. ASIA** Hii ni Tovuti ilengayo Asia na ina makala tofauti katika lugha nyingi za Kiasia, pia pamoja na makala mengine katika Kiingereza.
**CCOG. IN** Hii ni Tovuti inayolenga wale walio wa asili ya Kihindi. Inazo makala katika lugha ya Kiingereza na lugha zingine za Kihindi.
**CCOG.EU** Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Ulaya. Inazo makala katika lugha za Ulaya.
**CCOG. NZ** Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya New Zealand na wengine wa ukoo wa Uingereza.
**CCOG.ORG** Hii ndiyo Tovuti ya Kanisa la Mungu Linaloendela (CCOG). Inahudumia watu wa bara zote. Inazo makala, maunganisho, na video.
**CCOGCANADA.CA** Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya Canada.
**CDLIDD.ES** Hii ni Tovuti ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) **la Ufilipino**. Ina habari katika lugha ya Kiingereza na lugha ya Tagalog.

***Tovuti za Habari na Historia***

**COGWRITER.COM** Hii Tovuti ndiyo chombo kikubwa cha utangazaji na ina habari, mafundisho, makala ya kihistoria, video na visasa vya unabii.

**CHURCHHISTORYBOOK.COM** Hii ni tovuti rahisi ya ukumbusho na ina makala na habari za historia za kanisa.

**BIBLENEWSPROPHECY. NET** Hii Tovuti ya redio ya mtandao ambayo ina habari na mada za kibiblia.

**Idhaa za You Tube Video za Mahubiri na Mafundisho**

**BibleNewsProphecy** channel.CCOG sermonette videos.
**CCOGAfrica channel**.CCOG messages in African languages.
**CDLIDDSermones channel**.CCOG messages in the Spanish languages.
**ContinuingCOG channel**.CCOG video sermons.

# Ukuta wa awali wa Kanisa la Mungu la Mlima wa Maghabiri wa Yerusalemu.

Picha ya nyuma inaonyesha baadhi ya matofali machache yaliyobaki (pamoja na baadhi yaliyoongezwa baadaye) ya jengo katika Yerusalemu ambalo wakati mwingine huitwa jengo la pasaka la mwisho, lakini linaelezwa kama Kanisa la Mungu lililoko Mlima wa Magharibi wa Yerusalemu (ambapo sasa hivi huitwa Mlima wa Sayuni). fInaaminiwa kuwa eneo la jengo la kanisa la awali la Wakristo wa ukweli.

Matofali kutoka hekalu la Wayahudi yaliyoharibiwa na Warumi mwaka wa 70 B.K., yanaaminiwa ya kwamba yalitumika kujenga msingi na kuta za jengo hili.

Hadithi zingine zinapendekeza ya kwamba jengo/ukuta huu uko karibu na mahali ambapo pasaka ya mwisho ya Yesu, Pentecoste ya Matendo 2 na/ama matukio mengine ya Agano Jipya yalifanyika (kama Mathiya kuchaguliwa kuwa Mtume, Matendo 1:12-26).

Wakati matumizi yake ya Agano Jipya yanazua maswali ya kisayansi, historia inaonyesha kwamba lilitumika na Wakristo wa awali katika karne ya kwanza.

Hata hivyo, hili ndilo jengo katika Yerusalemu lililofundisha Injili ya Ufalme wa Mungu ambayo Yesu alifundisha (Marko 1:14-15).

Zaidi ya hayo, ni hakika kuwa ilikuwa eneo Wakristo walinda Sabato Wanazareti walitumia hadi walilazimishwa nje katika karne ya nne na wafuasi wa mtawala Constantino waliodai imani yake.

Ijapokuwa Wagiriki-Warumi wamekuwa wakijenga aina ya kanisa lao katika eneo hilo,baadhi ya matofali yanaendelea na yameonyeshwa kwenye jalada.Kanisa la Mungu Linaloendela (CCOG) linaendeleza Ukristo wa awali kwa imani ile na linakumbusha watu ya kwamba hiyo ya awali ilitokea Yudea na Yerusalemu kama ilivyofanya jengo lililojulikana na Wakristo.

*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma,... ndugu,mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi,katika Kristo Yesu.(1 Wathesalonike 2:13-14)*

*Mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. (Yuda 3).*

*Akawaambia (Yesu), Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa. (Luka 4:43)*

*Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ufalme. (Luka 12:31-32)*

*Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo mwisho utakapokuja. (Mathayo 24:14)*